MTIHANI WA MWIGO WA KAUNTI YA KAKAMEGA
Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)
102 / 1
KISWAHILI (INSHA)
KARATASI YA 1

1. Baa la mafuriko limekuwa donda ndugu katika taifa letu, Jopo la watu sita limeteuliwa kushughulikia tatizo hili. Wewe kama katibu wajopo hili, andika ripoti yenu.
2. Kazi mbi si mchezo mwema.
3. Namna ya kukwamua tatizo la njaa linalotuzonga kila uchao.
4. Kuwasili kwa Baraka na Malkia kulipokelewa kwa hisia mseto ... Endeleza kisa hiki.

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI YA KAKAMEGA
Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya (K.C.S.E)
102 / 2
KISWAHILI
Karatasi 2
Lugha

1. UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia

Uzalendo ni hali ya kuipenda nchi yako kwa moyo wa dhati. Mara nyingi viongozi wetu huhimiu vijana kuwa na uzalendo. Swali la kujiuliza ni hili: uzalendo huanzia wapi? Uzalendo lazima uanzie nyumbani. Kijana ama mtu yeyote ahakikishe kwamba anapenda nyumbani kwao. Kupenda nyumbani ni sawa na kupenda wazazi wako na kusikia maagizo wanayokupa mara kwa mara. Kljana sharti awe na nidhamu. Nithamu ikianzia nyumbani, vijana wetu bila shaka watakuwa na nidhamu shuleni. Wakufunzi wao hawatakuwa na matatizo na masharti wanayopewa na wakubwa wao basi migogoro shuleni, vyuoni, na hata kazini haitakuweko.

Kijana hawezi kuwa raia mwema ikiwa anadharau utamaduni wake. Kila kijana akumbuke kuwa mwacha mila ni mtumwa. Mila zetu, desturi zetu, madhebu yetu na imani zetu ndiyo nguzo ya raia mwema ambaye atashiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa, Kupenda utamaduni wa nchi yako ndio uzalendo tunaozungumzia. Vijana wetuwa leo ndio viongozi wetu wa kesho, Uzalendo ndio silaha ya pekee ya kuimarisha nchi yetu kisiasa, kitamaduni na kiuchumi.

Maovu yote yanayotukablli yataondolewa ikiwa vijana wetu watazingatia uzalendo kwa nchi yao. Ndiposa Rais wetu huwa anatuusia kuwa, yeyote anayejiingiza katika vitendo vya kuhujumu nchi yake si mzalendo. Falsafa ya mtu lazima iambatane na misingi ya kidemokrasia iliyokubaliwa na wote. Nchi yetu ni kama mama yetu.

Yule anayekashifu nchi yake ni sawa na kutukana mama yake. Mtu kama huyu huwa hana uzalendo wowote kwa nchi yake. Vijana wetu wajitoe mhanga kwa jino ukucha kupigania amani, upendo na umoja katika nchi yao.

Maovu mengine kama ufisadi, ukabila, uhasama, magendo pamoja na ulanguzi wa dawa za kulevya yataondolewa miongoni mwetu ikiwa tutazingatia swala la uzalendo. Watu wan a moyo wa tamaa. Tamaa ni kitu kibaya na wakati mwingine huzaa baa. Kuna watu ambao wanataka kujitajirisha kwa haraka bila kujali matakwa ya taifa. Watu kama hawa ni nadra sana kuzingatia maswala ya kitaifa. Ubinafsi ndio unaowatawala na aghalabu huwa wamefunikwa na wingu jeusi wasione mbele. Utamwona mtu kama huyo akiwa mbadhirifu wa fedha kwa kununulia watu pombe huku hafikirii kutoa chochote kuwasaidia wasiojiweza. Muungwana ni kitendo, hivyo ndivyo walivyosema wahenga wetu. Ikiwa watu matajiri hawataweza kusaidia au kuwajali wengine ambao hawakubahatika miongoni mwetu,basi matajiri kama hao hawana imani kwa nchi yao. Moyo wa kusaidia lazima uweko. Mchango wako kwa maendeleo waweza kuthaminiwa ikiwa uliutoa kwa moyo mkunjufu, kwani 'kutoa ni moyo, usambe ni utajiri'.

Sisi sote tuwe na nidhamu kazini. Tusijiingize katika vitendo vya kuibia serikali saa za kazi kwa lengo la kuyashughulikia maslahi yetu mengine. Tusiibe mali ya serikali huku tukitarajia serikali yetu kutufanyia mengi kwani kufilisisha serikali yetu ni sawa na kujifilisisha sisi wenyewe. Maovu haya tutayazika katika kaburi la sahau ikiwa tutaongozwa na moyo wa upendo kwa nchi yetu. Uzalendo ndio nguzo ya taifa lililo changa kama letu. Uzalendo utafanya nchi yetu kuwatajiri. Nafasi za kazi zitaongezeka, vijana wetu hawalakuwa na taabu ya kutatuta kazi. Ulitima utakuwa fti jambo Ia sabau. Sisi sote tuipende nchi yetu na tuwe layeri kuifta kwa vyoyyote.

Maswali

(a) Pendekeza anwani mwafaka ya kufaa makala haya. (alama **1)**
(b) Eleza maana ya neno uzalendo (alama 1)
(c) Kwa nini uzalendo unaliganishwa na silaha (alama 2)
(d) Andika maovu manne ambayo yataondoIewa miongoni mwetu iwapo yijana watazingatia uzalendo. (alama2)
(e) Kutoa ni moyo, usambe ni utajiri. Fafanua kwa muktadha wa habari hii. (alama 2)
(f) Je, migogoro shuleni husababishwa na nini? (alama2)
(g) Maovu katika jamii yetu yatakabiliwa vipi? (alama 2)
(h) Eleza maana ya matumizi yafuatayo ya lugha: (alama 3)

i) Ulanguzi
ii) Wajitoe mhanga.
iii) Wingu jeusi
iv) Ulitima
v) Falsafa
vi) Madhehebu

2. UFUPISHO

Soma makala haya kwa makini kisha ujibu maswali yote mawili yafuatayo:

Kila nchi duniani huwa na sheria zinazostahili kufuatwa iii kuweza kuongoza nchi hiyo. Sheria hizi ndizo jumla ya kanuni ambazo huwezesha serikali itawale na kuendesha shughuli zake za kila siku. Hii ndiyo katiba ya nchi.

Siasa ni itikadi inayofuatwa na kundi la watu ili kuendeleza maisha yao kwa jumla.Siasa nzuri huwezekana tu kukiwa na watu wanaoheshimu katiba yao; wakubwa kwa wadogo.

Nchini Kenya kwa mfano, katiba ya nchi humhitaji mtu kushiriki katika maongozi ya nchi pale anapotimia miaka kumi na minane. Katika umri huu, kila raia wa Kenya anastahili kusajiliwa na kupata kitambulisho cha kitaifa. Kitambulisho hicho humwezesha mtu huyo kutekeleza majukumu yake bila vikwazo. Kati ya majukumu hayoni kupiga kura ili kuchagua viongozi.

Katiba inatakikana ihifadhi asasi zote nzuri za raja na kuzilinda. Itambue tofauti za jamii mbalimbali na tamaduni zao kwa nia ya kuziheshimu huku ikilinda umoja wao wa utaifa. Kwa mfano, asasi ya mahakama iwajibike kutenda haki wala isitumiwe kuangamiza watu wake.

Nchi haiwezi kujiendeleza bila kushirikiana na nchi zingine za ulimwengu. Siasa na katiba ya nchi yoyote iimarishe mahusiano na wananchi wa sehemu mbalimbali iii kupata maendeleo na ufanisi.

Mabalozi wawe kiungo muhimu katika kufanikisha mahusiano haya.

Raia sharti wawe na njia za kujitafutia riziki. Siasa za nchi sharti zihakikishe wananchi wanapata ajira na nafasi za kujiendeleza. Kuwe na utaratibu ufaao wakati wa kuajiri wafanyikazi. Nao wafanyi biashara wapewe nafasi ya kujiendeleza vilivyo.

Muungano wa viongozi na raia wenzao huweza kuunda vyama vya kisasa na kugombea uongozi wana nchi. Vyama hivi ndivyo vyombo rasmi vya kuendeleza sera za uongozi katika mataifa mengi ulimwenguni. Kila chama hujaribu kupata nyadhifa za kuongoza serikali kwa nia ya kuimarisha maisha ya jamii,

Ili shughuli hizi zote zifanikiwe, ni sharti pawe na katiba itakayohakikisha usa lama katika hali na nyakati zote.

Siasa na katiba ni sura mbili za sarafu hiyo moja kwani ni jambo Iisiloweza kutengwa na hali halisi ya maisha ya raia.

Maswali

(a) Tumia maneno yapatayo 50 kufupisha aya ya kwanza hadi ya tatu
Nakala Chafu (alama 5)
Nakala Safi

(b) Tumia maneno yapatayo 75 kueleza mambo muhimu anayoyazungumzia mwandishi katika aya nne za mwisho
Nakala Chafu
Nakala Safi

3. <u>MATUMIZI YA LUGHA</u> **(alama 40)**

(a) Eleza matumizi ya 'kwa' katika sentensi hizi:

(i) Rashid alipanda mti <u>kwa</u> kasi

(ii) Ugatuzi ni mfumo unaopaswa kutekelezwa <u>kwa</u> utaratibu.. (alama 2)

(c) ***Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali.*** (alama 2)
Walikashifiwa kwa kuwa watundu sana

(c) ***Unda nomino kutokana na vitenzi hivi*** (alama 4)

(i) Onea

(ii) Umia

(d) ***Akifisha sentensi ifuatayo***
tukifika tutaagana na mjomba hamisi aishiye mombasa sakama hana haja yakuolewa ghana lengo lake kuu ni kusoma rafiki yake alisema. (alama 4)

(e) ***Onyesha viambishi awali na tamati katika sentensi hii ya neno moja:*** (alama 3)
Walishambuliwa

(f) ***Yakinisha sentensi hii;-*** (alama 2)
Baba hakunilipia karo wakati nilipokuwa nikisoma

(g) ***Tunga sentensi moja moja kudhihirisha matumizi ya:*** (alama 2)

(i) Mwayo

(ii) Mwasho

(h) ***Andika sentensi zifuatazo katika hali zilizo kwenye mabano.*** (alama 4)

(i) Kijikombe chake kilivunjika baada ya kuangukia kijigari (ukubwa)
(ii) Mtu yule haachi kuandamana na mbwa wake aliyedhoofika kiafya (udogo)

(i) ***Eleza maana zinazojitokeza katiku sentensi hizi:*** (alama 2)

(a) Waliuliwa wanyama
(b) Wanyama waliuliwa

(j) ***Andika sentensi moja kuthibitlsha mwingiliano wa maneno yafuatayo.*** (alama 3)
Nomino kuwa kivumishi

(k) ***Andika kwa wingi***
Mwiwa wangu alihukumiwa kifungo cha maisha (alama 2)

(i) ***Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea bila kutumia '-amba'*** (alama 2)
Mtu ambaye alifiwa ndiye ambaye aliomboleza zaidi

(m) ***Kamilisha methali zifuatazo:***
(i) Mgomba changaraweni (alama 2)
(ii) Mche mnyamavu

(n) ***Eleza maana ya nahau hizi:*** (alama 2)

(i) Mambo kujipa
(ii) Kosa macho

(0) ***Vinyambue vitenzi vifuatavyo kulingana na maagizo*** (alama 2)
(i) Ja (tendwa)
(ii) La (tendesha)
(iii) Nata (tendeshwa)
(iv) Juvya (tenda)

(p) Andika upya sentensi hizi bila kutumia kirejeshi - amba (alama 2)

(i) Ufisadi ambao umetusumbua kwa miaka na mikaka ndio ambao serikali mpya yapasa kukomesha.
(ii) Tarishi ambaye anakuja ni mchezaji stadi wa kandanda.

(q) Taja aina ya maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi hii: (alama 2)
Mwalimu mwadilifu huongoza wanafunzi wake vyema

4. **ISIMU JAMII** (alama 10)

(a) Eleza maana ya isimu Jamii (alama 2)
(b) Kwa nini watu hufanya makosa katika matumizi ya lugha? (alama 8)

MTIHANI WA MWIGO WA KAUNTI YA KAKAMEGA
Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
(FASIHI)
SEHEMU YA A: TAMTHILIA
Mstahiki Meya – Timothy Arege

1. Swali la kwanza (Lazima)
'… basi katusemee tena huenda akakusikiliza…diary yake imejaa…'

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (al.4)
b) Kwa nini mhusika anatambua mrejelewa awasemee? (al.2)
c) Eleza kwa kutolea mifano sifa za msemaji. (al.6)
d) Tambua na ueleze maswala mawili makuu aliyohitaji msemewa awasemee. (al.4)
e) Tambua na ueleze tamathali moja iliyotumika katika dondoo na ueleze jinsi ilivyotumika katika Tamthilia. (al.4)

SEHEMU YA B: RIWAYA
S.A. MOHAMMED: Utengano
Jibu swali la 2 au la 3

2. 'Mwanzo alidhani yeye kakamata mpini, lakini kumbe alikuwa kakamata makalini. Sasa ndiyo kwanza aone kuwa kisu kimemkatakata. '

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (al.4)
b) Ni tamathali zipi mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili? (al.4)
c) Ni vipi kisu kilimkata mrejelewa. (al.12)

au

3. ‘Malezi ya mtoto wa kike ni kizungumkuti’, thibitisha kwa kutoa mifano mwafaka kutoka katika Riwaya ya Utengano.

SEHEMU YA C : HADITHI FUPI

Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine

Jibu swali la 4 au 5

4. Jazanda ya samaki wa nchi za joto ni anwani faafu. Thibitisha. (al. 20)
5. Tofautisha usawiri wa mwanamke katika hadithi za **Damu nyeusi** na **Mke wangu** (al. 20)

SEHEMU YA D : USHAIRI

6. Soma shairi ulilopewa kwa makini kisha ujibu maswali.

Pindi ilipomjia, khabarii za binti kazaliwa,
Uso ulimsawijika kwa soni akachanganyikiwa.
‘Hii ni nukhusi?
Aka, ni nakama!
La, ni beluwa?”
Bali si beluwa?”

Wapi uso aufiche?
Au mchangani auzike?
Izara hii asiipate!
Ya kuzaliwa ‘mke’

Nitawatolea kisa
Nawatangulizia sasa,
Kisa kilichoanza,
Kinachoendelea hasa,
Baharini wala bara,
Kote kimeenea
Namna wanavyomtesa,
Kiumbe dhahili wamemnyanyasa,
Lini atathaminiwa?

Kisa chenyewe kitendawili,
Mwenye busara atoe taawili,
Ya haya mambo mawili,
Maisha bila ‘mke ni awali,
Kisa kingeendelea?
Lulu iliyohifadhiwa ni ya pili
Kisa kingeendelea?

MASWALI

a) Mshairi ana ujumbe gani katika shairi hili? (al.4)
b) Taja na ueleze tamathali ya lugha iliyotawala shairi hili (al.3)
c) Hili ni shairi la aina gani? Eleza (al.3)
d) Fafanua umbo la shairi hili ukizingatia: (al.4)
i) Ubeti
ii) Mishororo
iii) Mizani
iv) Vina
e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi. (al.3)
i) Beluwa
ii) Baharini wala bara
iii) atathaminiwa
f) Kwa nini akadkeza kuwa kisa kingeendelea? (al.3)

SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI

7. a) Ni nini maana ya ulumbi katika Fasihi Simulizi? (al.2)
   b) Fafanua umuhimu wa ulumbi.
   c) Taja na ueleze sifa nne za ulumbi. (al.8)

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA ZA UGENYA / UGUNJA, 2013
Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/1
KISWAHILI
KARATASI 1
Muda: Saa 1¾

1. **Insha ya lazima**
   Wewe ni mgombezi wa kiti cha ubunge katika eneo lako la bunge na unaamini ya kuwa mpinzani wako alitumia mbinu zilizosababisha wewe kushindwa. Andika barua kwa Tume Huru ya Mipaka na Uchaguzi ukiwasilisha malalamiko yako.
2. Eleza namna katiba mpya itakavyoleta mabadiliko mbalimbali katika nchi ya Kenya.
3. Bidii ya mja haiondoi kudura.
4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno yatuatayo :
   ... Bwana na Bi. arusi wakaondoka na kuwaacha waliohudhuria kula, kunywa na kusherehekea usiku kucha. Kweli mwanzo mwema huwa na mwisho mwema.

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA ZA UGENYA / UGUNJA, 2013
Cheti Cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/2
KISWAHILI
KARATASI 2
Muda: Saa 2½

1. **UFAHAMU (Alama 15)**
   Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali

Tangu asili na jadi nasikitika kusema kuwa tumekuwa tukiwakandamiza mabanati wetu na kuwateka bakunja ilhali wameonyesha kuwa wenye mikono miepesi. Siku moja nilikuwa nikitembea na babu yangu mkongwe tulipoliona tapo la wanawake kwa mbali. "Funika kombe mwanaharamu apite" akaninongo'nezea, kisha walipopita akaniambia, "'Hao ni viumbe duni wasiojitegemea. Wanahusudu uwezo tu." Kwa uchanga wangu wa fikra sikuelewa yakini alichotazamia lakini leo nang'amua. Basi imenibidi kuitupilia mbali dhana hiyo hafidhina kwani aisifuye mvua aghalabu imemnyea.

Jina zuri hung'aa gizani na bila shaka majina ya wanawake wetu yamemeremeta kama nyota. Kwanza, wamejitolea mhanga katika nyanja za masomo. Si haba ambao wamehitimu kutoka vyuo vikuu vya humu nchini na vilevile vya ughaibuni na kujipa shahada kadha wa kadha. Wamepata ujuzi kwa kutosha katika maswala kama vile udaktari na uanasheria. Hivi ni kumaanisha kuwa tuna madaktari shupavu, basi tuwape nafasi tusiendelee kuwa nyuma mithili ya koti katika kipengele hiki muhimu cha maisha. Ni wanawake ndio. lakini mgalla muue na haki umpe!

Vilevile wanawake wetu wamejitokeza mbele katika hatamu za uongozi. Mfano mwafaka ni katika serikali yetu, ambapo mawaziri kadhaa manaibu wa mawaziri na wabunge ni wanawake. Nani asiyefahamu Charity Ngilu, Dr. Julia Ojiambo, Beth Mugo na Martha Karua? Wote wanafanya bidii za mchwa kustawisha maisha ya wananchi.

Kwa upande mwingine wanawake ni walezi waliomakinika. Kama tujuavyo udongo upatilize ungali maji na usipoziba ufa huna budi kuujenga ukuta. Nani ndio wamepokezwa jukumu hili la malezi ? Nina zetu hujitolea kwa hali na mali kuwatunza watoto kwa tajiriba zinazofaa na kuwafunza maisha ndiposa wasifunzwe na ulimwengu. Aliyemakinika atakubaliana nami kuwa malezi si jambo la kufanyiwa mzaha katika harakati za ujenzi wa taifa. Na huu wajibu wote ni kwa wanawake.

Siwezi kuwasahau wanawake wanamuziki. Sote twaelewa kuwa kwa uchumi kama wetu, kutegemea kazi ya kuajiriwa ni kutaka muhali, chambilecho wahenga, mchagua jembe si mkulima. Nashukuru wanadada kwetu kwa kutia bidii katika uwanja wa muziki badala ya kuwa viruka njia. Kupitia kwa sauti zao nyororo kama kinanda wameweza kuwavutia hata watalii kuitembelea nchi yetu na kutuachia pesa za kigeni. Nawahimiza wcngi kama iwezekanavyo wajaribu bahati yao. Jambo hili linajuzu sana katika ujenzi wa taifa imara.

Katika kitengo cha spoti, wanawake wamejizatiti vilivyo na kutokea watanashati kwelikweli. Wamezika katika kaburi la sahau kuwa mchezo ni utawala wa wanaume. Kwa mfano katika michezo ya Olimpiki au Jumuia ya madola, timu zetu za wanawake zimefanya vyema na kurudi nyumbani na nishani chungu nzima. Kwa wale wasiohusika katika michezo ningewasihi wajikakamue kisabuni bali wasiwaonee kijicho wenzao kwani nyota ya mwenzio usiilalie mlango wazi. Iwapo tutazingatia ufanisi katika michezo, taifa hili halina budi kuendeleza uchumi wake.

Kwa kukunja jamvi, ningetaka kusisitiza kuwa hata ingawa jitihada haziondoi kudura, wanawake wetu wamefanya bidii za

kutosha na inafaa wapewe nafasi sawa na wanaume katika ujenzi wa taifa. Ningewahimiza wanaume wasiwe na kinyongo dhidi ya wanawake bali chanda chema kivishwe pete. Huu ndio mwito wangu na kama tujuavyo kuro haisemi uongo na mbiu ya mgambo ikilia haikosi ina jambo.

Maswali

a) Andika anwani mwafaka kwa taarifa uliyoisoma. (alama 1)

b) Eleza dhima ya mwanamke kwa mujibu wa taarifa hii. (alama 4)

c) Uchumi wa nchi waweza kuimarishwa kwa njia *gani* ? (alama 4)

d) Unafikiri ni kwa nini mwandishi asema, "Wamepata ujuzi wa kutosha katika maswala tatizo kama vile udaktari na uanasheria (alama 2)

e) Msimamo wa mwandishi kuhusu uana (jinsia) ni upi? Toa sababu. (alama 2)

f) Eleza maana ya vifungu vya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu hiki: (alama 2)

i) Vyuo vya ughaibuni

ii) Viruka-njia

2. MUHTASARI

Ubinafsishaji wa mashirika ya umma ni nguzo kuu katika ulimwengu wa leo. Kimsingi, ubinafsishaji ni hatua na harakati zinazochukuliwa kupunguza kushiriki kwa serikali katika uendeshaji wa mashirika na kuhimiza kupanuka kwa sekta ya kibinafsi.

Serikali huweza kuhimiza, kutokana na uuzaji, uhawilishaji wa mali kutoka umiliki wa umma hadi kwenye umilikaji wa sekta ya kibinafsi. Aidha, serikali inaweza kuuza hisa zake kwenye mashirika ya umma. Njia nyingine ni kuchochea ugavi wa zabuni kupitia kwa mikataba ambayo inashindaniwa na mashirika au kampuni tofauti. Lengo kuu la ubinafsishaji ni kuigatua nafasi ya serikali katika utendakazi na uendeshaji wa mashirika.

Uuzaji wa mashirika ya kiserikali au hisa huwa chanzo cha mapato yanayoweza kutumiwa kuendesha miradi mingine.Hii ni njia ya kupunguza harija ya serikali inayotokana na uendeshaji wa mashirika yasiyoleta faida. Ubinafsishaji huzuia uwezekano wa kuingiliwa kwa mashirika na wanasiasa. huimarisha utamaduni mpya wa muundo wa mashirika na huvunja uhodhi wa kiserikali. Ubinafsishaji huweza atika mbegu za ujasiriamali wa raia, kutamani kuanzisha amali tofauti.

Ubinafsishanji huweza kuyaruhusu mashirika va kimataifa kutwaa mashirika muhimu nchini, kufutwa kazi kwa wafanyi kazi na kuongezeka kwa umaskini. Ubinafsishaji wa sekta zinazohusiana na elimu na afya huweza kuathiri vibaya wenye mapato ya chini na ubinafsishaji haumaanishi ufanisi wa utendakazi wa makampuni na mashirika. Aidha, ikiwa haupo utaratibu mzuri wa kutathmini au kupima thamani za hisa pana uwezakano wa hisa zinazouzwa kupewa thamani ya juu au ya chini.

a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa kifungu, fanya muhtasari wa aya ya kwanza na ya pili.
(Maneno 35-40) (alama 5 utiririko1) (alama 6)
Matayarisho
Nakala safi

b) Dondoa hoja muhimu zinazojitokcza katika aya ya tatu na ya nne. (Maneno 45-50) (alama 7,2 ya utiririko) (jumla 9)
Matayarisho
Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

a) Eleza sifa bainifu za irabu */u/* (alama 2)

b) Eleza matumizi mawili ya koloni/nukta mbili (:) (alama 2)

c) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa wingi. (alama 2)
Mwizi aliiba kikapu na ngombe.

d) Andika sentensi hizi ukitumia mnyambuliko uliomo mabanoni. (alama 2)

i) Mwanafunzi yule ali .....dawa kwa urahisi (-pa. tendeka)

ii) Maziwa yote yata .....na mtoto yule. (-nywa. tendwa)

e) Kanusha sentensi ifuatayo : (alama 1)
Nitasoma na kulala

f) Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi zifuatazo.
Mtoto mwenyewe alienda shambani. (alama 1)
Kazi yetu haihitajiki shuleni (alama 1)

g) Tunga sentensi kuonyesha matumizi yafuatayo ya kwa: (alama 2)

a) Kifaa/chombo

b) Umilikaji

h) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo, (alama 2)

Kijana alianika nguo bola ya kupanga nyumba .

i) Bainisha vielezi na uelezc ni vya aina gani katika sentensi zifuatazo.

i) Mfanyakazi yeyote atakayefanya kazi kivivu atafutwa . (alama 2)

ii) Waliafikiana wakutane kwangu.

j) Andika katika usemi wa taarifa : (alama 2)

"Tutaleta maembe haya kesho iwapo mtakubali," Joel alisema,

k) Andika sentensi ifuatayo ukitumia kirejeshi tamati. (alama 3)

Mkulima aliyefanikiwa kilimoni ni yule aliyelima kwa jitihada na pia aliyetumia mbolea nyingi.

l) Unda kitenzi kimoja kwa kila nomino zifuatazo : (alama 2)

i) ghadhabu

ii) shupavu

m) Tambua aina za virai vilivyopigwa mstari. (alama 2)

i) Mtoto alinunuliwa mpira <u>mwingine mzuri</u>

ii) <u>Shambani mwake</u> mlipandwa mahindi.

n) Tunga sentensi moja kuonyesha tofauti kati ya vitate vifuatavyo :

Karama/ gharama (alama2)

o) Hainisha vitenzi vinavyopatikana katika sentensi hizi. (alama 3)

i) Mwanafunzi huyu si mwaminifu

ii) Mazingira yamekuwa yakihifadhiwa tangu jadi.

p) Ainisha sentensi ifuatayo ukitumia jedwali. (alama 4)

Mvulana mrefu anavuka barabara.

q) Andika sentensi hii katika hali sambavu. (alama 2)

Ondiek alicheza mpira.

r) Eleza maana va sentensi: (alama 2)

"Ningalikuwa na pesa ningalinunua nyumba na ningalistarehe"

s) Eleza maana ya pasi katika sentensi ifuatayo: (alama 1)

Alikula wali pasi kunawa mikono.

4. ISIMU JAMII

a) Lahaja ni nini? (alama 2)

b) Tajajinsi tatu za kupunguza tofauti za kilahaja. (alama 3)

c) Taja manufaa matatu ya lahaja. (alama 3)

d) Taja milano miwili ya lahaja za Kiswahili. (alama 2)

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA SHULE ZA KAUNTI YA VIHIGA-2013
Cheti Cha Kuhitimu Elimu Ya Secondari (K.C.S.E)
102 / 1
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA

1. Wewe ni kinara wa kidato cha 4 shuleni mwako. Wanafunzi wamekuwa na malalamishi kuhusu maandalizi yao kwa mtihani mkuu ujao. Andaa ripoti kuhusu malalamiko hayo.
2. Uchaguzi mkuu humu nchini mwaka huu ulikuwa na manufaa mengi kuliko hasara. Jadili.
3. Siku ya nyani kufa miti yote huteleza.
4. Andika insha itakayokamilikia kwa maneno haya:-
   .....wote waliwaza wakiwazua kwa huzuni, kijana akitetemeka mbele yao kwa huzuni na uchungu, ni uso gani usingetahayarika kumwona Songo akifunika usowe kwa fedheha! Nilitikisa kichwa na kuondoka pale polepole.

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA SHULE ZA KAUNTI YA VIHIGA-2013
Cheti Cha Kuhitimu Elimu Ya Secondari (K.C.S.E)
102 / 2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA

1. UFAHAMU **(alama 15)**

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali

Lugha imekuwa kikwazo kikubwa katika kukuza teknolojia ya habari na mawasiliano **(TEKNOHAMA)** barani Afrika. Lugha ambazo zimekuwa zikitumiwa ni za kimagharibi kama vile Kijerumani, Kifaransa na Kiingereza. Idadi kubwa ya Waafrika, hasa wanaoishi vijijini, hawazifahamu lugha hizi.

Uamuzi wa Shirika la Microsoft wa kutumia lugha ya Kiswahili katika programu za kompyuta kuanzia mwaka 2005 ni mchango mkubwa. 'Kuzinduliwa kwa mradi huu ni tukio la kipekee kuimarisha teknolojia sehemu za mashambani. Mradi huu umewawezesha wananchi takribani milioni 150 wa janibu za Afrika Mashariki kufaidi huduma za tarakilishi.

Utekelezaji wa mradi huu halikuwa jambo jepesi. Kwanza, ilibidi Shirika la Microsoft chini ya uongozi wa Bill Gates kulishawishi Bodi lake la wakurugenzi. Bodi liliposhawishika kuwa Kiswahili ni lugha inayotumiwa na mamilioni ya watu liliidhinisha kuzinduliwa kwa mradi. Hatua iliyofuatia ilikuwa kuteua maneno 700,000 ya kimsingi ya Kiingereza ambayo yangetafsiriwa kwa Kiswahili.

Hatua iliyofuata ilikuwa ushirikiano na dola pamoja na mashirika ya kibiashara na taasisi za kielimu ulimwenguni. Ilipobainika kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili yangehamasisha uwekezaji katika vituo vya mtandao vijijini, ushirikiano katika kuendesha mradi huu uliafikiwa bila shida. Mradi huu ulichukua muda wa miezi 18 kukamilika. Uliwashirikisha wahusika katika uwanja wa teknolojia ya habari, mawasiliano, elimu, biashara na idara za Kiswahili katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki. Vyuo vikuu hivi ni pamoja na Dar es Salaam, Nairobi, Kenyatta na Makerere,

Wataalamu walioshirikishwa walisaidia katika kubuni faharasa ya istilahi za Kiswahili 3,000. Hizi ni zile ambazo zinafaa kwa matumizi ya kompyuta ya kawaida na ya kila siku. Mradi huu umeshangiliwa na wakereketwa na wapenzi wa Kiswahili katika nyanja zote. Wasomi, wanariadha, wanamuziki, watalii, wafanyabiashara, wanasiasa, wafuasi wa dini mbali mbali na wakulima; wote wamefurahia hatua ya Kiswahili kuingizwa kwenye mtandao.

Watu ambao walikuwa hawawezi kuturisha tarakilishi kwa sababu ya kutojua Kiingereza sasa hawana kisingizio. Matumizi ya Kiswahili yatapanua na kuimarisha mawasiliano baina ya watu wanaoishi vijijini na pembe zote za ulimwengu.

Jambo la kutia moyo zaidi ni kuwa sasa vyuo vikuu vinavyotoa masomo kwa kutumia mitandao vimepewa idhini ya kutumia programu hizi. Walimu na wanafunzi wanapata habari moja kwa moja kwa Kiswahili bila kutafsiri. Kuna uwezekano sasa wa kusambaza mafunzo katika nyanja na viwango vyote kwa mfumo wa elimu ya mbali

Katika ulimwengu wa utandawazi, tukio kama hili lina manufaa makubwa. Wananchi wa vijijini wanaweza kupata habari na maarifa kutoka pembe zote za dunia na kuhusu masuala tofauti tofauti kwa lugha wanayoiclewa barabara.

Kusambaa kwa matumizi ya ngamizi vijijini kutaimarisha biashara inayofungamana na teknolojia ya mawasiliano. Hali hii itainua maendeleo ya kitcknolojia na kiwango cha maisha vijijini. Bila shaka **mwachano** uliopo baina ya sehemu za mijini na vijijini utapungua.

Haya ndiyo maendeleo anayokamia kila mja wa siku hizi. Lililopo ni serikali kupania kupanua na kusambaza muundo mbinu kama umeme na simu katika sehemu zote za nchi. Pamoja na haya, kuna haja ya kupunguza bei ya ngamizi na vipuri vyake ili kuwatia motisha watu kununua kompyuta kwa wingi. Ikumbukwe kuwa lengo la kuanzisha mradi huu lilikuwa kuisaidia serikali kupanua na kusambaza matumizi ya huduma za kompyuta na mtandao katika shule, vituo vya kijamii na mancno ya makaazi. Huduma hizi ni msingi wa elimu, biashara na mawasiliano ya kisasa.

Maswali

(a) Eleza hatua zilizotekelezwa ili kuingiza Kiswahili katika mtandao. (ala. 4)

(b) Lugha imekuwa kikwazo kikubwa katika kukuza teknolojia ya habari na mawasiliano barani Afrika. Thibitisha kauli hii. (ala.2)

(c) Fafanua faida za mradi wa kutumia Kiswahili katika ratiba ya tarakilishi. (ala.3)

(d) Serikali inahitaji kufanya nini zaidi ili kufanikisha mradi huu? (ala. 3)

(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyo tumiwa katika taarifa. (ala.3)

i) Faharasa

ii) Wakereketwa

iii) Ngamizi

2. UFUPISHO

Soma makala haya kisha ujibu maswali

Aibu kubwa ya taifa kushindwa kukabiliana na tatizo sugu la ajali za barabarani bado inaendelea kuwafedhehesha wahusika katika sekta ya uchukuzi na mawasiliano licha ya matumizi ya vidhibiti mwendo na kanda za usalama.

Ajali za barabarani zinaangamiza idadi kubwa ya watu kila mwaka wakiwemo viongozi na watu mashuhuri. Miongoni mwa sababu ambazo zinaleta maafa barabarani pamoja na uendeshaji kasi kupita inavyotakikana, yaani kukiuka masharti yalyowekwa na wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano. Madereva wengi hung'oa vidhibiti mwendo vilivyowekwa, hawarekebishi mikanda ya usalama, wala hawayapeleki magari yao kukaguliwa mara kwa mara kama inavyopaswa. Yale yanayopelekwa kwa ukaguzi, mengi hushindwa kutekeleza kanuni zilizowekwa kwa hivyo hutegemea hongo kuwa barabarani.Fauka ya hayo, madereva wa malori na matrela mara nyingi huendesha magari hayo wakiwa walevi. Dawa za kulevya, kama miraa na bangi hutumiwa sana na hawa na matokeo yake huwa ajali mbaya.

Hata hivyo, lawama haiwezi kuelekezewa madereva pekee. Ukiangazia barabara nchini Kenya utapata kuwa barabara haziko katika hali nzuri. Zile za lami zimekuwa na mashimo makubwa ambapo mvua ikinyesha hufanya vidimbwi mithili ya michimbo ya madini yaliyojaa maji baada ya kuachwa wazi. Na zile barabara zisizokuwa na lami zimcharibika kiasi kwamba ni vigumu kuzitofautisha na njia za ng'ombc kwenye maeneo kame kinachohitajika ni kuzirudisha katika kiwango ambacho zitaweza kufaa tena.

Wananchi pia inafaa waelimishwe iIi wasikubali kupanda magari ambayo tayari yamejaa. Hili litawasaidia wananchi wenyewe kudumisha usalama wao barabarani. Pia inawafaa watambue ya kwamba wanajukumu la kuwaarifu walinda usalama endapo dereva anaendesha kwa kasi kuliko ile ya kilomita themanini kwa saa iliyokubaliwa. Inafahamika kuwa maafisa wa usalama ndio wafisadi zaidi, hivyo basi huchangia katika kuongeza idadi ya vifo barabarani. Katika vita vya ufisadi na ajali za barabarani ni mwananchi mwenyewe ambaye atawezesha kukomesha hali hii. Kwa mfano, afisa wa usalama akipatikana akichukua hongo, yeye pamoja na yule aliyetoa hongo wakamatwe na kupelekwa kwenye vituo vya kukabiliana na ufisadi na kuchukuliwa hatua kali, matatizo haya yataisha. Lakini kabla kufikia hapo, ni muhimu kumhamasisha mwananchi kuhusu haki zake na namna ya kukabiliana na suala hili la ufisadi. Hali hii inatuonyesha kwamba mipango maalum inapaswa kufanywa na serikali ili kuwaelimisha wananchi kama hatua ya kwanza kukabiliana na ufisadi hatimaye izilainishc sekta zotc wala Si ya uchukuzi na mawasiliano pekee.

Maswali

a) Eleza mambo yote muhimu anayozlingumzia mwandishi katika aya ya pili na tatu. (maneno 50) (ala 8)
   Nakala chafu
   Nakala safi

b) Bila kubadilisha maana iliyokusudiwa, fupisha aya ya mwisho. (**maneno 40)** (ala.7)
   Nakala chafu
   Nakala safi

3. MATUMIZI VA LUGHA:

a) Ainisha mofimu katika kitenzi hiki:
   Hawakufiwa. (ala 3)

b) Hizi ni konsonanti za aina gani na zinatamkiwa wapi? (ala.4)

	Aina	Mahali pa kutamka
i) ch		
ii) f		

c) Andika kwa udogo na wingi
   Ndege huyu alimla kifaranga (ala.2)

d) Onyesha kishazi huru na tegemezi katika sentensi hii
   Ijapokuwa kulikuwa na baridi kali niliondoka kwenda sokoni . (ala.2)

e) Bainisha vitenzi katika sentensi hizi na ueleze ni vya aina gani.

i) Ouma amekuwa uwanjani . (ala.2)

ii) Huyu ndiye mwalimu mkuu .

f) Yakinisha.

Hakula chakula wala kunywa maji . (ala.2)

g) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo.
Mvulana huyo alikashifiwa mno kufeli mtihani wa kitaifa . (ala.2)

h) Eleza matumizi matatu tofauti ya 'ki ' (ala.3)

i) Sahihisha sentensi ifuatayo: (ala.2)
Mama mwenye alikufa amezikwa katika makaburini

j) Eleza maana mbili za sentensi hii: (ala.2)
Alitimua mbio kuona ndovu

k) Bainisha shamirisho tofauti katika sentensi fuatao:
Ali alimnunulia simu mpenzi wake. (ala.2)

l) Changanua sentensi fuatayo ukitumia mehoro wa matawi
Mwanafunzi huyu anaandika vizuri sana. (ala. 4)

m) Huku ukitoa mifano fafanua miundo minne ya majina katika ngeli ya U - ZI. (ala 4)

n) Andika kwa msemo wa taarifa. (ala.2)
"Lo! Umeweza kuubeba mzigo huu pekeyo?" Mama Alishangaa.

o) Nyambua vitenzi vfuatavyo katika kauli ulizopewa. (ala. 2)

Kitenzi	Kutendea	Kutendana
(i) la (ii) paka		

p) Tunga sentensi ukitumia alama zifuatazo za kuakifisha. (ala.2)

(i) Ritifaa

(ii) Koloni/nukta pacha

4. ISIMU JAMII **(alama 10)**

1. a) Taja na ufafanue nadharia zinazoelezea chimbuko la lugha ya Kiswahili. (ala.6)
   b) Eleza hatua serikali inachukua kuipa lugha ya kiswahili hadhi ya kuwa lugha ya taifa. (ala. 4)

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA SHULE ZA KAUNTI YA VIHIGA-2013

Cheti Cha Kuhitimu Elimu Ya Secondari (K.C.S.E)

102 / 3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI.

Swali la lazima

1. a) Eleza maana ya hekaya (al. 2)
   b) Tambua sifa zozote sita za hekaya. (al. 6)
   c) Fafanua dhima ya hekaya katika jamii. (al. 6)
   d) Thibitisha kuwa kuna udhaifu katika uhifadhi wa fasihi simulizi. (ala.6)

SEHEMU B : TAMTHILIA

Mstahiki Meya- Timothy M. Arege.

Jibu swali la 2 au 3

2. .. . (Akicheka) shinikizo lililokuwepo lingetuua.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)

b) Ni shinikizo gani zilizokuwepo ambazo zingeweza kuwafisha wahusika. (al. 6)

c) Eleza namna mhusika huyu na wenzake walivyochangia kusababisha shinikizo ambazo zingewaua. (al. 10)

3. Jadili mbinu alizotumia mstahiki Meya kuendeleza uongozi wake cheneo. (al. 20)

SEHEMUC: RIWAYA

Utengano: Said A Mohamed

Jibu swali 4 au 5·

4. Kuna nini? Naskia zogo tu: 'Kuna nini enn?

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)

b) Ni nini kilichotokea kablana baada ya dondoo hili. (al.6)

c) Eleza uhusika wamsemaji katika dondoo. (al. 6)

d) Yaliyotokea kabla ya dond60hili yanaonyesha aina fulani ya Utengano. Fafanua. (al. 4)

5. Huku ukitumia mifano maridhawa, onyesha jinsi mbinu ya taharuki inavyotumiwa katika riwaya ya Utengano: (al. 20)

SEHEMU D: USHAIRI

6. ***Soma mashairi yafuatayo kasha ujibu maswali.***

SHAIRI A

Nimeona, milima na mabonde, misitu na nyika,
Nimeona, majani na umande, uliotandazika,
Nimeona, mkulima yuwenda shambani.

Nimeona, uwanda na magugu, yalomkabili,
Nimeona, wa jibu na vurugu, wiano mkali,
Nimeona mkulima akiwa tayari.

Nimeona; kwa ari na juhudi, anatupa jembe,
Nimeona.'Kakaza ukaidi, kwa nguvu achimbe,
Nimeona, mkulima akiwa kazini.

Nimeona kija kinawaka, kama jehanamu**!**
Nimeona, jembe lainuka, linapohujumu,
Nimeona, mkulima akiwa mbioni.

Nimeona, mvua yamiminika, naye- hatohisi,
Nimeona, kwa kani anatimka, bila wasiwasi,
Nimeona, mkulima akiwa kazini.

Wakati miaka inaibwa mmoja mmoja
Kurudi nyuma, kusimama, kupunguza mwendo,
Siwezi nyuma, kusimama, kupunguza mwendo,
Mtelemko mkali huu,
Lini na wapi mwisho sijui.

Mbele chui mweusi, nyama mwanga
Nionako kwa huzuni vifirushi maelfu vya dhambi,
Kisu, maisha kafiri haya,
Kama kutazama nyuma au mbele,
Ni kufa moyo mzima.

Sasa kama simba- mtu shauri nimekata
Ya nyuma sana nisijali ya mbele sana, niyakabili,
Kwa ujasiri na uangalifu nitazunguka,
Kila pigo wa moyo wangu,

Huu mpigo muziki wa maisha,
Na sioni jashoIinapomwaika, yendapo mazao,
Na sioni hadbiye kutukuka, yendapo mazao,
Kwa nini? Nauliza mkulima; kwani?

SHAIRI B

Maswali

a) Linganua mashairi haya:
(i) Kimundo
(ii) Kimaudhui. (al. 8)
b) Tambua kwa mifano mwafaka idhini tatu uhuru wa mshairi katika tungo hizi. (al.3)
c) Andika ubeti watatu wa shairi A katika lugha ya nathari. (al. 3)
d) Tambua toni ya mwandishi katika mashairi A na B. (al. 4)
e) Mafungu haya yametumiwa kwa maana gani katika mashairi haya. (ala.2)
   (i) Kakaza ukaidi
   (ii) Simba - mtu

SEHEMU E: HADITHI FUPI

Damu nyeusi na Hadithi nyingine- K. W Wamitila

7. "Mwakumbuka miaka miwili iliyopita? Bwana mtajika alivunja masharti ya kikaza nasi tukafanya hisani na huruma."
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (ala. 4)
b) Ni masharti yapi aliyovunja Bwana mtajika. (al. 4)
c) Mwandishi amemtaja Bwana mtajika kama kiongozi mwenye uwezo wake. Tambua huu uwezo. (al. 4)
d) Mbali na neno kikaza ambalo limetumiwa kijazanda, tambua jazanda zingine nne katika hadithi na ufafanue. (al. 8)
8. Wanawake ni viumbe wa kujitakia makuu. Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi zozote kumi katika Damu nyeusi na hadithi nyingine. (al. 20)

TATHMINI YA SHULE ZA UPILI ZA JIMBO LA MERU, 2013
KIDATO CHA 4
Cheti Cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/1
KISWAHILI
KARATASI 1
Muda: Saa 1¾

1. Wewe ni katibu wa chama cha Kiswahili shuleni mwenu. Andika ripoti ya mwisho wa mwaka 2012.
2. Eleza hatua zinazochukuliwa na serikali kumshirikisha mwanamke katika maendeleo ya jamii ili kuleta usawa wa kijinsia.
3. Mpanda ngazi hushuka.
4. Andika insha inayomalizika kwa:
   ... tulipoangalia nyuso zao tulijua kwa kweli tulikuwa tumeshindwa vibaya katika mchezo huo.

TATHMINI YA SHULE ZA UPILI ZA JIMBO LA MERU, 2013
KIDATO CHA 4
Cheti Cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/2
KISWAHILI
KARATASI 2
Muda: Saa 2½

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Kuanzia sasa madereva watakaosababisha vifo kwa kutokuwa waangalifu barabarani watafungwajela maisha.

Nao wale ambao watapatikana na hatia ya kucndesha magari wakiwa walevi watatozwa faini ya ksh.500,000, kifungo cha miaka 10 au adhabu zote mbili.

Hizi ndizo baadhi ya adhabu kali zilizoko katika sheria mpya ya Trafiki iliyotiwa saini na Rais Mwai Kibaki mnamo Alhamisi wiki hii.

"Mtu atakayepatikana na hatia ya kuendesha gari akiwa mlevi au baada ya kutumia dawa za kulevya atahukumiwa kifungo kisichozidi miaka 10 au atozwe faini isiyozidi sh.500,000 au apewe adhabu zote mbili," inasema sheria hiyo imetokana na marekebisho yaliyofanyiwa sheri a ya Trafiki ya hapo awali. Yeyote atakayepatikana akiendesha gari bila leseni pia atapokea adhabu kama hiyo.

Waendeshaji pikipiki za bodaboda nao hawajasazwa. Wao pia watahitajika kuwa na leseni na kofia maalum na jaketi inayoakisi mwangaza.

Abiria wao pia watahitajika kuvalia kofia na jaketi aina hiyo. Atakayepatikana na hatia ya kukiuka shuruti hili ataadhibiwa kwa kutozwa faini ya sh.l0,000, jela mwaka mmoja au adhabu zote mbili.

Sheria hii inajiri wakati ambapo nchi hii imezongwa na ongezeko la ajali za barabarani ambazo kiwango kikubwa husababishwa na makosa ya kibinadamu kama vile uendeshaji wa magari kiholela.

Takwimu kutoka idara ya Trafiki yaonyesha kuwa watu wanane hufariki huku wengine 20 wakijeruhiwa kila siku kwenye ajali za barabara.

Kwa jumla watu takriban 3000 hupoteza maisha yao katika ajali za barabarani kila mwaka, asilimia 23 ya vifo hivyo vikisababishwa na magari ya uchukuzi wa abiria. Majuzi sekta ya kibinafsi, chini ya uongozi wa kampuni ya simu ya rununu, Safaricom na chama cha wamiliki wa vyombo vya habari, ilizindua kampeni ya kitaifa inayolenga kupunguza ajali za barabarani chini ya kauli mbiu "TOA SAUTI".

Kupitia mpango huo wananchi wanahamasishwa kutoa habari kwa maafisa wa usalama wanaposhuhudia vitendo vyovyote vinavyohatarisha maisha ya watumiaji barabara.

"Madereva pia watahitajika kutahiniwa upya baada ya miaka miwili iii kubaini ikiwa bado ni weledi katika utendakazi wao," inasema sheria hiyo.

Vilevile, sheria hiyo inampa Inspekta mkuu wa polisi mamlaka ya kutenga maeneo ambapo vizuizi vya barabara vitapaswa kuwekwa, na kuondolea mbali mwenendo wa sasa ambapo polisi wa Trafiki huweka vizuizi bila mpango maalum. Inatarajiwa kuwa sheria hii itapelekea kupungua kwa visa vya ajali barabarani humu nchini.

Maswali

a) Ipe taarifa uliyoisoma anwani mwafaka. (alama 1)
b) Eleza sababu za ongezeko la ajali barabarani. (alama 4)
c) Taja aina za adhabu zinazotolewa na sheria mpya ya trafiki. (alama 4)
d) Mbali na sheria za trafiki ni njia zingine zipi zinazoweza kupunguza ajali za barabarani? (alama 3)

e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu: (alama 3)
i) hawajasazwa ii) shuruti iii) mwenendo

2. MUHTASARI: (alama 15)

Utalii ni sekta muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Mamilioni ya watalii huzuru nehi yetu kila mwaka ili kuja kujionea mandhari ya kuvutia pamoja na mbuga za wanyama zenye ufahari wa kimataifa. Wanyama wa mbugani wanaopatikana ni kama vile ndovu, kifaru, twiga, simba, chui na ndege kama vile kongoni, flamingo, tai, mbuni na kadhalika. Wanyama hawa na ndege huwavutia sana watalii kiasi eha kuwapiga picha kuzihifadhi ili wafikapo makwao waweze kuwaonyesha jamaa zao ambao nao huingiwa na shauku ya kutaka kuvinjari katika nehi yetu ya Kenya.

Watalii wanapofika nchini huimarisha pato kubwa kutokana na fedha nyingi za kigeni wanazoipatia nchi hii kama ushuru. Wanapotembelea mbuga za wanyama pia hutoa ada fulani ya fedha ambazo husaidia kuongeza pato letu la kiuchumi. Katika hoteli au mikahawa wakulima humu nchini hupata fursa ya kuyauza mazao yao kama vile mboga, matunda, mayai, nyama na kadhalika na kupata riziki zao. Vijana wengi ambao wamekuwa wakirandaranda mitaani hupata nafasi za ajira za kazi mbalimbali kama vile unajimu, upishi, ulinzi, ukalimani na kadhalika. Wengine huajiriwa kama madereva au waelekezi wa watalii hawa. Watalii pia huimarisha uhusiano mwema baina ya nchi yetu na nchi tofauti tofauti wanazotoka. Uhusiano huo hudumisha amani na utangamano nchini. Watalii hawawezi kuzuru nchi ambayo inakosa amani.

Hata hivyo, kama waswahili walivyosema hakuna mehele hukosao ndume. Shughuli za utalii katika nchi yetu zimetuletea madhara si haba. Baadhi ya watalii huja nehini na kuleta mila na desturi zao ambazo si nzuri sana. Kwa mfano, watalii mara nyingi hawaoni haya wanapotembea wakiwa nusu uchi huku wakishikana mikono na kupigana pambaja hadharani. Haya ni mambo ya kustaajabisha hasa sisi Waafrika. Baadhi ya vijana nao hujiingiza katika uhusiano wa kimahaba na watalii hao wa kike na hata wa kiume. Huu ni utovu wa nidhamu kwa vijana wetu.

Licha ya watalii kutuletea fedha nyingi za kigeni tunaona kuwa faida tunayopata kutoka kwao si nyingi sana. Kwa mfano, watalii husafiri kwa ndege zinazotoka mashirika yao. Hata mahoteli wanamolala na kulipia ni ya mashirika ya kutoka janibu za huko ugenini. Magari wanayosafiria watalii pia ni ya makampuni ya kutoka kwao kama vile 'Pollmans' 'Ust' 'Francorossaco ' 'UTC' na kadhalika.

Ingekuwa bora kama watalii wote wanaotaka kuingia nehini wawekewe masharti ya kusafiri kwa shirika la ndege la 'Kenya Airways'. Wafikapo hapa wajipumzishe na kustarehe katika mahoteli yanayomilikiwa na wakenya. Kisha wasafirishwe kwa kutumia usafiri wa umma kama vile magari ya 'matatu'. Hapo ndipo tutakapoweza kupata faida kemkem kutokana na utalii.

Tukitazama kwa makini tutaona kuwa faida za utalii ni ehache kuliko hasara zake. Hata hivyo, utalii si lazima uwe wa wageni peke yake hata wakenya wanaweza kuwa watalii.

<u>Maswali</u>

a) Fupisha aya ya kwanza na ya pili. (Maneno 55-60) (alama 8, utiririko 2)
Matayarisho / Jibu

b) Eleza madhara ya utalii kama yanavyojitokeza kuanzia aya ya tatu hadi ya nne.
(Maneno 35-40) (alama 4, utiririko 1)
Matayarisho / Jibu

3. MATUMIZI YA LUGHA: (alama 40)

a) Tofautisha sauti hizi: (alama 2)
i) /t/ ii) /z/

b) Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya nomino katika ngeli ya ku-ku (alama 2)

c) Andika sentensi itakayodhihirisha matumizi mbalimbali ya 'po' (alama 2)

d) Andika maana ya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)
Wahandisi hao walikarabati <u>barabara</u> hiyo <u>barabara</u>.

e) Tunga sentensi kuonyesha kishazi huru na tegemezi. (alama 2)

f) Yakinisha: (alama 2)
Asingefika mapema asingempata

g) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo katika mabano. (alama 2)
i) ja (tendewa)
ii) oa (tendesha)

g) Bainisha virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
<u>Watoto hawa</u> wameimba <u>vizuri sana .</u>

h) Andika kinyume eha sentensi ifuatayo : (alama 2)
Mwalimu alipoingia darasani wanafunzi walisimama.

i) Tambua aina za shamirisho katika sentensi hii : (alama 3)
Mwalimu aliandikiwa insha kwa kalamu.

j) Andika katika udogo (alama 3)
Mti huo uliangukia nyumba ya mvulana

l) Andika katika usemi wa taarifa: (alama 2)
"Niitie watoto wangu wote kesho," baba aliomba.

m) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama 2)
KN (N + V) + KT (T + E)

n) Akifisha: (alama 3)
salaale umewahi kumwona ngombe kondoo au mbuzi mwenye miguu mitatu .

o) Ainisha mofimu katika neno: (alama 3)
sijakuletea

p) Eleza matumizi ya 'ji' katika sentensi hii : (alama 2)
Mfugaji alijikata kidole

q) Jaza jedwali (alama 4)

Kitenzi	Kivumishi	Nomino
Boresha		
Safisha		

4. ISIMU JAMII: (alama 10)

Mtu I: Habari customer.
Mtu II: Mzuri bwana. Leo nimefika mapema.
Mtu I: Hivyo ni poa sana. Nikuletee nini?
Mtu II : Chai ya mkandaa na silesi mbili tafadhali.

a) Tambua sajili inayorejelewa na mazungumzo haya. (alama 2)
b) Tambua Mtu I and Mtu II (alama 2)
c) Fafanua sifa tatu za sajili hiyo zinazojitokeza katika mazungumzo haya. (alama 6)

TATHMINI YA SHULE ZA UPILI ZA JIMBO LA MERU, 2013
Cheti Cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/3
KISWAHILI
KARATASI 3
Muda: Saa 2½
SEHEMU A : USHAIRI

1. Lazima
Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Wakati umewadia, kwa hamu tulongojea,
Mtihani mefikia, kwa kasi bila kujua,
Muda wenu metimia, nyumbani mwaelekea
Fanaka nawatakia, mfanyao mtihani

Mengi mumejisomea, kwa bidii kuzitia,
Semi mukazichambua, methali kusimulia,
Ngeli mkazipangia, kwa fasaha fundishia,
Fanaka nawatakia, mfanyao mtihani

Dakika za mwisho sikia, ni bora ninawambia,
Uzembe ndugu kataa, za mchwa wenza kuthia,
Kusoma kuwe ni nia, akilini zingatia,
Fanaka nawatakia, mfanyao mtihani

Walimu kuulizia, swali gumu kujibua,
Bongo lako kuliona, mtihani shambulia,
Mijadala kuandaa, ushindi kuuthukua,
Fanaka nawatakia, mfanyao mtihani

Jalali Mola Jalia, dua zetu pokea,
Mwanga kuwamulikia, gizani sije bakia,
Elimu kuzidishia, fahamu kuwapatia,
Fanaka nawatakia, mfanyao mtihani

Wanafunzi nawausia, matapeli wamejaa,
Gomba na kuwauzia, kidhani wasaidia,
Kumbe wawaharibia, matokeo kufutia,
Fanaka nawatakia, mfanyao mtihani

Kile kilichobakia, ni akili kutumia,
Na muombeni Rabia, mlosoma kubakia,
Karatasi kipokea, ujaze bila udhia,
Fanaka nawatakia, mfanyao mtihani

Tisini zimetimia, uwanja nawaachia,
Anyolewapo sikia, chako kichwa maji tia,
Yaillah yajalia, waongoze njema njia,
Fanaka nawatakia, mfanyao mtihani

a) Je, ni nini dhamira ya mshairi ? (alama 2)
b) Eleza muundo wa ubeti wa nne wa shairi hili. (alama4)
c) Huku ukitoa mifano mwafaka eleza mifano miwili ya uhuru wa mshairi. (alama 4)

d) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari. (alama 4)
e) Onyesha tamathali ya usemi moja iliyojitokeza katika shairi hili. (alama 2)
f) Fafanua toni ya shairi hili. (alama 2)
g) Eleza maana ya mancno haya: (alama 2)
i) udhia
ii) matapeli

SEHEMU B : HADITHI FUPI
Ken Walibora na Said A. Mohamed: Damu nyeusi na Hadithi Nyingine
Jibu swali la 2 au la 3

2. "Ahaa! Alikuwa dereva mzungu na alipokuona akafikiria wewe ni jambazi?''
a) Fafanua muktadha wa dondoo hili.
b) Andika tamathali inayojitokeza katika dondoo hili.
c) Eleza maafa yaliyomfika msemewa baada ya mazungum zo haya.
d) Andika sifa zozote tatu za msemaji. (alama 6)

3. "Tahadhari kabla ya kutenda"
Jadili ukweli wa methali hii ukirejelea hadithi ya kanda la usufi. (alama 20)

SEHEMU C: TAMTHILIA
Timothy M. Arege: Mstahiki Meya
Jibu swali la 4 au la 5

4. "... sauti ni sauti tu! Wasemao mchana, usiku watalala."
a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b) Sauti zinazorejelewa zimcsababishwa na nini? (alama 12)
c) Mnenaji huyu alitoa ushauri gani mwingine katika tamthilia. (alama4)

5. Eleza huku ukitumia mifano mwafaka mbinu za kimtindo zifuatazo zilivyotumiwa katika tamthilia ya Mstahiki Meya.
a) Taharuki (alama 10)
b) Jazanda (alama 10)

SEHEMU D : RlWAYA
Said A. Mohamed: Utengano
Jibu swali la 6 au la 7

6. "Ulimwengu umenitoa woga ... na niogope nini, na hapa hapana simba."
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Andika tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)
c) Eleza jinsi ulimwengu ulivyomtoa msemaji woga. (alama 6)
d) Fafanua umuhimu wa msemewa katika riwaya ya Utengano. (alama 6)
7. "Jamii ya Utengano imekosa maadili." Jadili. (alama 20)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. **a**) Jadili matatizo yoyote matano yanayokabili ukusanyaji wa fasihi simulizi. (alama 10)
b) Eleza maana ya istilahi zifuatazo katika Fasihi simulizi (alama 6)
i) Maghani
ii) Ngomezi
iii) Misimu
c) Fafanua sifa zozote nne za maigizo. (alama 4)

JARIBIO LA MATAYARISHO YA K.C.S.E WILAYA YA GEM, 2013
KIDATO CHA NNE
Cheti Cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/1
KISWAHILI
KARATASI 1
Muda: Saa 1¾

1. Mwandikie mkurugenzi wa kampuni ya Safaricom barua ukiomba kazi ya uhandisi iliyotangazwa katika gazeti la "Taifa Leo" na uambatanishe wasifukazi wako.
2. Usalama umekuwa ukidorora katika taifa lako. Wewe kama katibu wa jopo la kuchunguza suala hili, andika ripoti ukieleza chanzo cha utovu huu wa usalama na upendekze njia za kuimarisha usalama.
3. Sanda ya mbali haiziki.
4. Andika insha inayoanza kwa maneno haya:
   Sasa ilikuwa zogo si zogo, vilio si vilio…….

JARIBIO LA MATAYARISHO YA K.C.S.E WILAYA YA GEM, 2013
KIDATO CHA NNE
Cheti Cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/2
KISWAHILI
KARATASI 2
Muda: Saa 2½

1. UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali chini yake

Kiswahili ni lugha ya taifa la Kenya. Wananchi wengi nchini Kenya huongea lugha ya Kiswahili. Ni dhahiri shahiri kuna makabila zaidi ya arobaini na mawili humu nchini.

Makabila haya huwa na lugha za ndimi za mama au lugha asili zinazotumiwa. Makabila haya yote huletwa pamoja na lugha ya Kiswahili.

Kiswahili kimeenea kote nchini Kenya hata hivyo ni tofauti mijini tukilinganisha na mashambani. Mijini, wakenya wamechukulia Kiswahili kama lugha ya wote inayozungumzwa na kila adinasi.

Mashambani Kiswahili ni lugha ambayo inavutia kila mtu. Wakenya mashambani wanazidi kukipa Kiswahili kipaumbele. Watu wanaozungumza lugha hii huonekana kuwa waliosoma.

Kiswahli kinachozungumzwa mijini ni cha aina gani? Jameni, utashangaa kama si kumaka utakapokutana na watu wawili wakijadiliana katika lugha ya Kiswahili sanifu kule mijini.

Lugha hii imechafuliwa na lugha inayoibuka na kugeuka mithili ya rangi ya kinyonga na kuenea kila uchao. Sheng' ni lugha ambayo imeathiri lugha teule ya Kiswahili pakubwa sana. Vijana wa mijini huona kuwa huzungumzi sheng'basi wewe umepitwa na wakati. La ajabu ni kuwa hata wazazi na watu wengine wazima ambao yafaa wawe vielelezo nao pia wamejiunga na klabu hii ya sheng.'

Hivi ni tofauti na mashambani ambapo vijana wengi hujibidiisha kuzungumza Kiswahili saf ingawa kuna athari za matamshi kwa sababu ya lugha za mama. Wavyele na watu wengine wazima pia hutumia Kiswahili chema kule mashambani kwani wanakubali kuwa Kiswahili ni lugha yenye adabu na heshima nyingi.

Kulingana na matokeo ya mtihani wa Kiswahili wa kitaifa kila mwaka, ni wazi kabisa wanafunzi wa mashambani hufanya vyema kuliko wale wa mijini. Jambo hili huwa ni la kukera sana hasa unapolinganisha matokeo ya Kiswahili na ya lugha nyingine kama kingereza kule mijini. Mbona wanafunzi waache mila zao kwa kutopenda lugha ya asili yao? Wakenya wapendwa, wakenya wazalendo tunawasihi mkienzi Kiswahili, ni kama titi la mama ambalo huwa tamu daima dawamu.

Walezi mijini wamekichukulia tu Kiswahili hivi hivi,

Hawajali Kiswahili kinachozungumzwa na wanao. Wengine wamedhani kuwa Kiswahili hufundishwa tu shuleni. Dhana hii ni potovu sana. Kipindi kimoja hakitoshi vile vipindi vya mwanafunzi akiwa na wenziwe kule mitaani wakikikandamiza Kiswahili kwa kutumia sheng'.

Mwalimu anapofundisha Kiswahili sanifu tuseme kwa muda wa saa moja na robo halafu mwanafunzi apatane na wenziwe na hata jamaa zake, wazungumze sheng' kwa muda wa saa tano mengine yanakosekana kama huyu atafika aendapo kweli? Yaani ataweza kuelewa lugha hii vyema kweli?

Kule mashambani, Kiswahili kimepewa hadhi yake vilivyo. Lugha hii hufunzwa mara ya kwanza shuleni. Mzazi anaposikia ati mwanawe ameanza kuzungumza Kiswahili basi yeye hujazwa na furaha ghaya huku akimtia mwanawe motisha. Hivi basi huyu mwana hukienzi Kiswahili na kutaka kukimanya ipasavyo,

Hivi majuzi kumekuwa na mjadala kuhusu kulifanya somo la Kiswahili kuwa la hiari shuleni. Ingawajambo hili halikueleweka vyema, ukweli ni kwamba penye moshi hapakosi moto. Huenda nijambo ambalo lilikuwa limewaziwa na mtu au

watu fulani. Haya ni maajabu kama mizungu. Yaani tuidharau lugha yetu na kuienzi lugha ngeni? Mimi sikubali hata chembe.

Nawaomba wazalendo wapiganie Kiswahili kwajino na ukucha. Chako ni chako. Nyumbani ni nyumbani. Heri mkate mkavu wa nyumbani kuliko nyama shwari ya pengine. Tusiuwache mbacha wetu kwa mswala upitao.

Maswali

a) Taarifa hii yafaa anwani gani? (alama 1)
b) Mwandishi wa makala ana mitazamo miwili kuhusu lugha ya Kiswahili. Itaje kwa kuitolea mifano. (alama 2)
c) Kiswahili kina changamoto nyingi kulingana na kifungu hiki, Zionyeshe. (alama2)
d) Makala yanadokezea juhudi gani za kufaharisha Kiswahili? (alama 3)
e) Tashbihi iliyotumiwa kifunguni ina maana gani? (alama 2)
f) Nini maana ya:
Tusiuwache mbacha wetu kwa msala upitao. (alama 2)
g) Taja visawe vya maneno haya:- (alama 2)
i) hadhi
ii) wavyele
iii) Dhana

2. UFUPISHO: (alama 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Unyanyasaji wa kijinsia umeongezeka kwa kiasi kikubwa kwenye shule zetu na katika taasisi za elimu, Mimba na ndoa za mapema kwa wasichana wanafunzi zinachangia asilimia 31 na 32 ya wasichana wanaoacha shule mapema kwenye shule za msingi za mashambani na mijini. Kitaifa mimba na ndoa za mapema zinachangia asilimia 31.3 ya wasichana wanaoacha shule kwenye shule za msingi. Jambo hili huchangiwa na visa vya unyanyasaji wajinsia kwa wasichana walio shule na walio nje ya shule hizo.

Unyanyashaji wa kijinsia ni jambo lisilovutia, linalodhoofisha hadhi ya mhusika, hali ambayo wasichana na wavulana hukumbana nayo katika maisha ya shule. Mbali na kulazimishwa kufanya tendo la ndoa, unyanyasaji ni vitendo vya dhihaka, maombi ya kufanya mapenzi na wahusika, kugusa sehemu zisizokubalika, kumpatia mhusika barua ama ujumbe ambao hautakikani na kudhalilisha kwa kuchora.

Waathiriwa mara nyingi huteseka kimya kimya hasa kama wako katika shule moja ambayo wametendewa unyama huo. Unyanyasaji wa kijinsia huathiri wavulana na wasichana kisaikolojia na kimwili. Unadhalilisha, kushusha hadhi na kuwaaibisha waathirika. Kwa sababu ya mitazamo na mila zisizofaa katika jamii ya Waafrika kama vile ndoa za lazima, kuwaona wanawake kama vifaa vya ngono, unyanyasaji wa kijinsia mara nyingi huonekana kamajambo la kawaida na mara nyingi hautilii maanani kutokomezwa. Wasichana ndio walio hatarini zaidi kuathiriwa na unyanyasaji huu na hivyo kuwaweka katika uwezekano mkubwa wa kupata mimba wakiwa wadogo na kuambukizwa magonjwa ya zinaa na ukimwi, hali inayopelekea kuporomoka kwa kiwango chao cha elimu, kubaguliwa, kuacha shule na wakati mwingine kifo.

Kuna shinikizo kubwa kwa wavulana pia, kimila na kutoka kwa wenzao kuwashawishi wafanye mapenzi ili kuthibitisha "Uanaume au ubingwa" wao. Kwa sababu ni wanaume, jamii inawatarajia kukabiliana na shinikizo hilo. Kwa hivyo, hakuna utaratibu wa kuwasaidia wavulana kukabiliana na shinikizo hili.

Mifumo mingi ya elimu haizungumzii maswala ya unyanyasaji wa kijinsia katika mafunzo ya ualimu, kwa hivyo, walimu hawana ujuzi na mbinu za kugundua na kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia darasani ama hata kutambua athari zake katika kufundisha na kujifunza, Walimu hawana budi ila kuunda mazingira mazuri ya darasani ambayo hayana aina yoyote ya unyanyasaji wa kijinsia. Walimu pia wanatakiwa waeleze bayana kuwa hawatavumilia ama kukubaliana na unyanyasaji wa aina yoyote; iwe darasani ama katika mazingira ya shule.

Serikali na mashirika mengine yasiyo ya serikali yanafaa kulitadarukia swala la unyanyasaji wa kijinsia, Hii ni kwa sababu kufikia sasa hakujawa na mikakati kabambe ya kulikomesha kabisa swala hili. Wengi wa wahasiriwa hawajui nani wa kumwendea katika hali kama hii, hivyo basi, wanaotekeleza unyama huu hawaajibishwi.

Maswali

a) Fupisha aya mbili za kwanza(maneno 50-55) (alama, 7, utiririko 2)
Matayarisho
Jibu
b) Ukirejelea aya nne za mwisho, dondoa mambo yanayochangia unyanyasaji wa kijinsia(maneno 45 -50)
Matarisho (alama 5,utiririko 1)
Jibu

3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)

a) i) Onyesha tofauti kati ya konsonanti zifuatazo. (alama 2)

/p/
/b/

ii) Taja kikwaruzo/kikwamizo ghuna cha ufizi. (alama 1)

b) Eleza matumizi ya 'po' katika sentensi zifuatazo: (alama 3)

i) Anapotembea Jane huimba.

ii) atembeapo Jane huimba

iii) Atembeapo Jane pana nyimbo.

c) Onyesha dhima ya kila mofimu iliyopigiliwa mstari. (alama3)

i) Ukinimbia kwa furaha utabarikiwa na Mola ambaye ndiye mwenye uwezo duniani.

d) Unda vitenzi kutokana na maneno haya uliyopewa. (alama 2)

i) Hojaji

ii) -rembo

iii) ahadi

iv) uwoga

c) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi hii. (alama 2)

Mto uliofurika unavukika sasa.

f) Andika sentensi hizi upya kwa maagizo uliyopewa mabanoni.

i) Nitakaa wakati utakapofunga mlango wa mama (kinyume) (alama 1)

ii) Nomino hii imeendelezwa visivyo. (ukubwa) (alama l)

iii) Ukitaka cha mvunguni sharti uiname.(wingi) (alama l)

iv) Joan alituzwa kwa kupasi mtihani. (wakati ujao hali timilifu) (alama 1)

v) Watoto ambao walikuwa wagonjwa wamepona. (kanusha) (alama l)

vi) Mimi sitakuwa na haja ya kumtolea wazo.

(yakinisha kwa wingi) (alama 1)

vii) Mwanafunzi alikuwa na matatizo mengi. Mwanafunzi alipasi mtihani (anza kwa licha ya ....) (alama 1)

g) Onyesha miundo yoyote miwili ya nomino za ngeli ya A-WA huku ukitoa mifano. (alama 2)

h) Tunga sentensi moja moja ukitumia neno '-zuri' kama. (alama 3)

i) Nomino

ii) Kiwakilishi

iii) Kielezi

i) (i) Andika neno moja lenye konsonanti mwambatano na uionyeshe, (alama 1)

(ii) Taja neno moja lenye silabi funge kisha uionyeshe . (alama 1)

j) Geuza katika usemi halisi. (alama 3)

Mwalimu alimwuliza mwanfunzi wake iwapo alikuwa amekamilisha tamrini naye akamjibu kwamba alikaribia kuikamilisha .

k) Tumia neno "alikuwa" katika sentensi kama.

i) Kitenzi kisaidizi

ii) Kitenzi kishirikishi

l) Tumia neno 'tupa' mara mbili kwenye sentensi moja ili kutoa maana mbili tofauti. (alama 2)

m) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi.

Wanafunzi wanaotaka kuanguka mtihani hulala darasani. (alama 4)

n) Taja aina za vihusishi vilivyopigiliwa mstari. (alama 1)

Sara aliwasili nyuma ya mhubiri na akanywa sharubati zaidi ya wenzake.

o) Maneno yaliyopigiliwa mstari yanatoa dhana gani? (alama 1)

i) Hesabu jinsi hii hukokotezeka kwa urahisi.

ii) Uamuzi wa daawa iliyowasilishwa mahakamani utakubaliwa na kila Mkenya ikiwa utakuwa wa haki.

4. ISIMU JAMII **(alama 10)**

a) Taja lahaja zozote mbili za kiswahili na uonyeshe eneo ambapo kila mojawapo inazungumzwa. (alama 2)

b) Taja na ueleze mambo yoyote matatu yaliyochangia maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya kabla ya uhuru. (alama 3)

c) Ewe Mola mtukufu mwenye mapenzi kwa viumbe vyote; mwenye kutoa neema kubwa kubwa na ndogo ndogo, wabariki hawa kondoo wako ....

i) Taja sajili ya kauli hii. (alama 1)

ii) Eleza sifa zozote nne za sajili hii. **(alama 4)**

JARIBIO LA MATAYARISHO YA K.C.S.E WILAYA YA GEM, 2013

Cheti Cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)

102/3

KISWAHILI

KARATASI 3

Muda: Saa 2½

A. FASIHI SIMULIZI

1. **a**) Eleza mbinu zozote nne za kukusanya data katika fasihi simulizi. **(alama 4)**

b) Fafanua matatizo yanayokwamiza utafiti na uhifadhi wa fasihi simulizi. **(alama 16)**

B. RIWAYA -UTENGANO - S.A MOHAMMED

Jibu swali la pili au la tatu

2. " .... sirudi bibi, na hasa nimeshakuwa debe bovu ... "

a) Eleza muktadha wa maneno haya. **(alama 4)**

b) Eleza mbinu moja ya luhga iliyotumiwa katika dondoo. **(alama 2)**

c) Onyesha ukweli wa dondoo kuwa anayezungumza amekuwa debe bovu. **(alama 6)**

d) Eleza nafasi ya mwanamke kwa mujibu wa riwaya ya Utengano. **(alama 8)**

3. Mfanyakazi katika jumuiya ya Utengano amedhalilishwa. Jadili. **(alama 20)**

C. MSTAIHKI MEYA

Jibu swali la 4 au 5

4. Haki zake mfanyakazi wa Baraza la cheneo zimekiukwa. Eleza **(alama** 20)

5. "Haraka haraka haina baraka. Usisahau kuwa Mstahiki Meya mwenyewe amesema."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Ukizingatia Tamthlia nzima, thibitisha kuwa ndugu Sosi hakustahili Umeya. **(alama 16)**

D. DAMU NYEUSI

6. **a)** Kuna masaibu mengi yaliyomkumba Fikirini alipokuwa Marekani kwa masomo zaidi. Eleza. **(alama 10)**

b) Pesa ndieho ehanzo eha maovu yote katikajamii, Jadili ukizingatia hadithi "Samaki Wa Nchi Za Joto. **(alama 10)**

E. USHAIRI

7. A: Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Tufanye kazi

Kila kiongozi wetu, amesema waziwazi,
Kazi iwe raha yetu, masila na kiangazi,
Wala pasiwe na mtu, anayefanya upuzi,
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu.

Huyo ni adui yetu, asotaka kazi,
Japo ana kila kitu, elimu pia ujuzi,
Kuwa naye sithubutu, huyo sawa na pwaguzi,
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu,

Ili hasidi si mwenzetu, kamwe hatumpongezi,
Kapotea lengo watu, kwani halitekelezi,
Harambee wito wetu, maana yake ni kazi,
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu,

Awe mshona viatu, jozi baada ya jozi,
Anawafaida watu, nyumbani na matembezi,
Akishona jozi tatu, hujipatia gawazi,
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu.

Dereba mbeba watu, nahodha mwenye jahazi,
Tabibu na sina zetu, pamoja na viongozi,
Hao tengemeo letu, sio kama majambazi,
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu.

Walimu ni nuru yetu, kwa masomo na malezi,
Hasirifu njia zetu, kuwapinga hatuwezi,
Wafunze tupate utu, maarifa na ujuzi,
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu.

Ukulima hapa kwetu, ndiyo kazi yamalezi,
Kilimo ni haki yetu, kunde shai na viazi,
Tulime tupate vitu, chakula na matumizi,
Mzembe katika kazi, huyo ni adui yetu.

Maswali

a) Toa kichwa kingine mwafaka kwa shairi **(alama** 1)
b) Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi. **(alama** 5)
c) Taja vikundi vinne vya watu ambavyo vimehimizwa kufanya kazi. **(alama** 4)
d) Eleza muundo wa shairi hili. **(alama** 4)
e) Katika ubeti wa mwisho, kwa nini mshairi akasema kilimo ni haki yetu? **(alama** 1)
f) Andika ubeti wa sita kwa lugha ya nathari. **(alama** 4)
g) Eleza maana ya neno - "anawazi ' kama lilivyotumiwa katika shairi. **(alama** 1)

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA – KAUNTI YA EMBU, 2013
Cheti Cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/1
KISWAHILI
KARATASI 1
Muda: Saa 1¾

1. Umaskini umekithiri sana katika kata yako. Andika barua kwa mahariri wa gazeti la Mwanga ukipendekeza hatua mahsusi za kupambana nao.
2. Serikali ya ugatuzi ina faida nyingi kuliko hasara. Jadili.
3. Mwiba wa kijichoma hauambiwi pole.
4. …Nilishusha pumzi nikashukuru; ama kweli niliokolewa kutoka pindo la chatu.

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA – KAUNTI YA EMBU, 2013
Cheti Cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/2
KISWAHILI
KARATASI 2
Muda: Saa 2½

1. UFAHAMU

Soma taarifa kisha ujibu maswali

Baada ya kesi kusikilizwa Kotini alifungwa miaka minne na kazi ngumu, sonara na mweka rahani kila mmoja alipata kifungo cha miaka miwili na miezi sita. Humo gerezani hawakuwa wakikaa pahali pamoja. Walikuwa wakilala vizimba mbalimbali. Walikutana asubuhi walipokuwa wakihesabiwa na kugawiwa kazi.

Siku hizo mahabusu wakifanyishwa kazi za nje na ndani. Humo kazini walisimamiwa wasitoroke. Iliwalazimu mahabusu kuwalinda ila siku za Jumamosi na Jumapili. Siku kama hizo walipumzika humo gerezani. Kazi za nje zikikuwa kuchimba, kuvunja na kuchonga mawe; vilevile kukata miti na kuni mwituni. Mahabusu wengine walipelekwa kulima na kufyeka nyasi kwenye nyumba za wafanyikazi wa serikali. Kazi za ndani hazikuwa kama hizo. Mahabusu wa kazi za ndani walifagia humo gerezani na vile vile walisafisha vizimba na kufua nguo.

Kotini siku hizo alikuwa na umri wa miaka ishirini na mitano. Kazi yake hapo kifungoni ilikuwa ya nje. Yeye na wenzake walipelekwa kwenye mwamba wa mawe kuehimba, kuvunja na kuchonga mawe. Walipewa sururu, mitaimbo, mashoka na karai kwa kazi hiyo. Mahabusu hao walifanya kazi juani, mvuani na baridini.

Hapo mwambani, Kotini alipenda zaidi kuchimba mawe. Alikamata sururu na mtaimbo kwa kazi hiyo. Aliweza kuchimba na kuvunja mawe mengi kwa juma moja. Siku nyingine, Kotini alifanya kazi ya kuvunja na kuchonga mawe kwa shoka vile vile Hapo mwambani, mahabusu hao walikuwa wakipokezana na wakisaidiana kazi. Baada ya kila juma, yalifika magari hapo chimboni kuyaondoa mawe hayo. Mahabusu waliyabeba mawe yaliyochongwa vichwani. Mawe ya mapande na kokoto waliyatia karaini halafu waliyabeba na kuyatia magarini. Mawe kama hayo yalitumika kwa kujengea majumba na barabara na mengine yakiuzwa,

Ilikuwa desturi mara nyingine mahabusu kubadilishwa kazi. Siku zilipofika, Kotini alibadilishwa kazi akapelekwa mwituni kukata miti na kuni. Kotini alikuwa mvulana mwenye afya nzuri na misuli mwilini mwake. Alipandezwa zaidi na kazi ngumu ya dharuba na sulubu. Hapo mwituni, alitumia shoka na msumeno kwa kukatia miti. Aliweza kuikata na kuibwaga miti minene na miembamba, mirefu na mifupi bila ya taabu. Siku hizo miti kama hiyo ikitumiwa kwa kujengea, mingine ilipasuliwa mbao na kutengenezewa milango, madirisha, masanduku na samani za nyumba, mingine ilifanywa kuni ambazo zikitumika kwa kupikia.

Idara ya Gereza liwafanyisha kazi mahabusu wote ili zipatikane pesa za kuweza kuwasaidia watu hao kwa chakula. Mawe, miti na mbao, vitu hivyo viliuzwa na pesa zikitumika kwa kuwalishia wafungwa hao. Idara hii haikuwa ikiwalisha bure wakosa kama hao bali ikiwatumia ili wajilishe wenyewe na kupunguza gharama za matumizi ya pesa juu yao.

a) Ipe taarifa uliyoisoma kichwa mwafaka. **(alama 1)**
b) i) Taarifa hii inarejelea watu wangapi? Wataje. **(alama 2)**
ii) Unafikiria wahusika uliotaja walifungwa kwa kosa gani? **(alama 2)**
c) Ni kwa nini wafungwa hawakulindwa siku za Jumamosi na Jumapili? **(alama 2)**
d) Ni kazi gani walizozifanya wafungwa? **(alama 3)**
e) Kazi za mahabusu zina manufaa gani? **(alama 3)**
f) Eleza maana ya maneno yafuatayo. **(alama 2)**
i) Sururu
ii) Desturi

2. <u>UFUPISHO</u> **(alama 15)**

Sehemu muhimu ya elimu tamaduni ilikuwa ile ya maisha ya asisi ya ndoa. Vijana, wake kwa waume, kwanza walifunzwa umuhimu wa asasi hii ya ndoa kwajamii. Waliaswa dhima adimu ya kujiheshimu kimwili kabla ya kuolewa ama kuoa. Elimu hii iliufanya kuwa mwiko na aibu kwa msichana kupata mimba nyumbani, au kwa mvulana kumtunga mimba msichana kabla ya ndoa. Kwa hivyo shida ya kuwepo kwa watoto haramu haikuzagaa katika jamii. Mafunzo kuhusu mpango wa uzazi yalikuwa muhimu. Ilikuwa ni aibu kwa mume na mkewe kuzaa watoto kabla ya miaka miwili au zaidi kupita. Wakati wa kunyonyesha mtoto, mume na mke walitarajiwa kutoonana kimwili, na hii ilisaidia katika kumlea mtoto.

Vijana waliaswa kuhusu kuchagua wachumba wao kwa kuelezwa ni ukoo au mbari gani ingefaa kuoa au kuolewa nao. Hili liliepusha kuwepo kwa ndoa baina ya watu wanaohusiana kinasaba. Elimu ya ndoa pia iliangazia sifa ambazo vijana walifaa kuchunguza kwa waandani wao kabla ya kufunga pingu za maisha nao. Kilichokuwamuhimu ni maadili au tabia, ndiposa ikasemekana kuwa 'uzuri wa mke ni tabia, si nguo.' Kadhalika, elimu hii ilihimiza kuwa shughuli ya uteuzi wa wachumba ishirikishe wazazi wa pande zote mbili iii kujenga mlahakana uhusiano bora baina yajamii husika za vijana waliopanga kuoana. Ndoa zote basi zilihitaji vibali vya wazazi wa mume na mke. Haya yalipunguza shida za mizozo na kuvunjika kwa ndoa.

Mambo sasa yamebadilika na elimu tamaduni ikapuuziliwa mbali. Tukichunguza asasi ya ndoa hivi leo kwa jicho pevu, tutabumbua mambo mengi ya kushtusha. Ndoa na mapenzi yaliyoitwa umoja wa masikilizano ya kinyumba sasa yamegeuzwa na vijana wa leo yaitwe uhayawani, dosari, kutosikilizana,~l:Ilumiana na hata kutoana uhai. Tumeshuhudia na kusoma kwa vyombo vya bahari jinsi ndoa zinavyodhulumiana, kujeruhiana na hata kutoana uhai!

Vyanzo vya matatizo katika ndoa ni chungu nzima.Kwa mfano, vijana wengi hujiingiza katika ndoa kwa pupa itokanayo na mvuto wa kijazba kwa urembo wa waandani wao. Wao husahau kuwa urembo wa ujana ni moshi, na utokapo kwa mpito wa miaka haurudi Ndiposa ndoa nyingi huvunjika kutokana na kutoaminiana baina ya wachumba. Wengine nao hawajatofautisha ndoa na ngono.

Wao hufunga ndoa kwa azma finyu ya kujitosheleza kimapenzi, wana ari ya kibinafsi ya kutaka kujiokoa kwa nafsi zao zinazoteketea kwa kiu ya ngono. Hatimaye hawakumbuki kujenga ndoa kwa misingi mipana. Wengine nao hupuuza majukumu yao ya ndoa kama mume na mke. Vijana wengi hasa wa kiume wamejitosa kwa ulevi uliopindukia na kusahau kuzishughulikia na kukimu mahitaji ya familia zao.

Kwa upande wao, vijana wa kike nao waolewapo na iwapo wanafanya kazi kama mabwana zao, hao huwa kwa thuluthi kubwa ya maisha yao, wanajitegemea na kujiona kama wanaishi na mabwana zao kama ada tu, bali wana uhuru wa kutenda vyovyoe vile wapendavyo. Iwapo wake wa namna hii watakemewa, hutisha kuwa watawaacha mabwana au kila mmoja wao awe na sehemu ya utawala katika nyumba zao, maana kila mmoja anaeho mwenziwe alichonacho. Bwana ana pesa - bibi anazo, bwana ana gari - bibi analo, bwana ana digrii bibi anazo nyingi na kadhalika. Hatima ya ushindani huu ni kuvurugana kunakosababisha talaka kwa ndoa.

a) Ukirejelea aya tatu za kwanza, eleza umuhimu wa ndoa katikajamii ya kale. (maneno 60-65) **(alama 6)**
Matayarisho:
Nakala safi:

b) Bila kupoteza ujumbe, fupisha aya mbili za mwisho. (maneno 70-75) **(alama 9)**
Matayarisho:
Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA **(alama 40)**
a) Tofautisha kati ya sauti ghuna na sauti sighunalhafifu. **(alama 2)**
b) Eleza maana mbili za neno mboni. **(alama 2)**
c) Ainisha
Kilichopikika **(alama 3)**
d) Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya ngeli ya: **(alama 2)**
i) KU
ii) I - ZI
e) Andika kwa wingi

Uwanja mwingine umechimbwa kuongeza urefu wake **(alama 2)**

f) Onyesha matumizi ya kwa katika sentensi hizi. **(alama 3)**

i) Tulifanya kazi kwa bidii

ii) Nyaga alikwenda hospitalini kwa matibabu.

iii) Sakaja alikula ugali kwa mkono.

g) Tunga sentensi moja katika wakati uliopita hali ya kuendelea. **(alama 2)**

h) Yakinisha sentensi ifuatayo.

Hatujakubaliana tuachane na tofauti zetu za kifamilia **(alama 1)**

i) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano. **(alama 3)**

i) Ziba (tenduka)

ii) tanda (tendama)

iii) Fumba (tendata)

j) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi.

Abiria waliojeruhiwa sana walipelekwa hospitalini. **(alama 4)**

k) Tunga sentensi kudhihirisha matum izi ya mshazari. **(alama 2)**

I) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa.

Fatuma aliscma, "Sofia aliniletea nguo ambayo nitavaa kesho." **(alama 2)**

m) Unda nomine kutokana na nomino hizi. **(alama 2)**

i) mvuvi

ii) uchaguzi

n) Andika kwa udogo.

Mguu wake umeoza baada ya kuumwa na nyoka. **(alama 2)**

0) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo.

Mama alimeza dawa yote na kumshukuru dada . **(alama 2)**

p) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo:

Kinyua anayecheza nafasi ya katikati anapendwa na wengi. **(alama 2)**

q) Tunga sentensi ifuatayo ukitumia. **(alama 4)**

i) Bighairi ya (kama kihusishi)

ii) Lau (kama kiunganishi)

4. ISIMU JAMII

Naona wengine wenu wamedanganywa na baadhi ya wagombeaji. Siku hiyo ikifika tathmini vizuri kabla ya kufanya uamuzi,

a) Tambua sajili ya lugha iliyotumika. **(alama 2)**

b) Fafanua sifa nne za sajili hiyo. **(alama 8)**

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA – KAUNTI YA EMBU, 2013

Cheti Cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)

102/3

KISWAHILI

KARATASI 3

Muda: Saa 2½

SEHEMU

1. LAZIMA

Kua.
Sikia.
Angalia.
Bongo tum ia.
Hadaa dunia.
Mwelevu hutulia.
Mwenye pupa huumia,
Papariko zina udhia.
Sura si kitu kujivunia.
Ukiwa hujafa hujatimia.
Mcheza na tope humrukia.
Asiyetosheka mtumwa wa dunia.
Roho mtoro ipendapo kukimbilia.
Sudi si ya kulilia, sikuye huwadia.
Watu wote ni sawa hakuna duni kwa Jalia.

Achekapo mwenye meno kibogoyo huungulia.
Zaidi mtu apatavyo ndivyo tamaa huzidia.
Uangaliapo mbele yako na kando yako angalia.
Katika kuishi na wenzetu, sharti tuwe twavumilia.
Hakuna mtoto wa haramu vitendo ndivvo haramia,
Pasi na viganja viwili kofi haliwezi kulia.
Sikiliza ya wengi bali lako peke shikilia.
Binadamu ni wa ila hapana alotimia.
Asiyeridhika ni fukara kupindukia.
Uongo sawa, ukweli watu hususia.
Hakuna raha kamili kwenye dunia.
Ajali huwezi kuitambikia.
Ungali hujatenda fikiria.
Maisha ni ya kuyanyatia.
Mali siyo ya kuringia.
Utu bora ni tabia.
Dh iki kuvum ilia.
Sipende kulia.
Shika wasia.
Fikiria.
Wazia. Tua.

a) Shairi hili ni la aina gani? **(alama 1)**
b) Taja lengo la mshairi. **(alama 2)**
c) Kwa nini utungo huu unachukuliwa kuwa shairi? **(alama 3)**
d) Eleza jinsi mshairi alivyoshughulikia dhana zifuatazo: **(alama 6)**
i) Tamaa
ii) Bahati
iii) Umaskini
e) Kwa kutoa mifano, onyesha mbinu mbili za kifasihi zilizotumiwa na mshairi. **(alama 4)**
f) Ni ipi hadhira lengwa ya shairi hili? **(alama 2)**
g) Eleza maana ya msamiati ufuato: **(alama 2)**
i) Jalia ii) Ila

SEHEMU B: RIWAYA

Said A. Mohamed: Utcngano

Jibu swali la 2 au la 3

1. "Kaa kitako, bibi haina haja ya kupandisha mori, hata majirani watakusikia. Tumejia heri, ikageuka shari"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
b) Kwa nini bibi huyu alipandisha mori? **(alama 6)**
c) Eleza vipi tukio hili ni heri kwa msemaji. **(alama 2)**
d) Onyesha njia nne zilizotumiwa kusuluhisha mgogoro huu. **(alama 8)**

au

3. Onyesha jinsi haki za watoto zimekiukwa katika riwaya ya Utengano. **(alama 20)**

SEHEMU C: TAM THILl A

Timothy Arege: mstahiki Meya

Jibu swali la 4 au la 5

4. "Ninalotaka kusema ni kwamba sikumbuki kushiriki ... ongezeko hilo ... "

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
b) Eleza matokeo ya mazungumzo hayo. **(alama 10)**
c) Fafanua sifa za mzungumziwa katika dondoo hili. **(alama 6)**

au

5. a) Eleza vikwazo vitano Wanacheneo walivyokumbana navyo katika harakati za kujikomboa. **(alama 10)**
b) Onyeshajinsi maudhui ya usaliti yanavyojitokeza katika tamthilia ya Mstahiki Meya. **(alama 10)**

SEHEMU D:

HADITHI FUPI Ken Walibora na Said A. Mohamed Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine

6. "Mwandishi wa hadithi ya kikaza amefaulu katika kutumia mbinu ya jazanda."
Thibitisha ukweli wa kauli hii. **(alama 20)**

SEHEMU E:

FASIHI SIMULIZI Jibu swali la 7 au la 8

7. a) Eleza maana ya ngano. **(alama 2)**

b) Fafanua sifa za ngano. **(alama 18)**

8. **a)** Misimu ni nini? **(alama 2)**

b) Eleza sifa tano za misimu. **(alama 10)**

c) Eleza umuhimu wa misimu katikajamii. **(alama 8)**

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA GUCHA KUSINI
Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya (K.C.S.E)
102 / 1
KISWAHILI
KARATASI YA KWANZA

1. **LAZIMA**
   Andika barua kwa mwenzako / rafikiyo anayeishi Uingereza na umweleze faida zinazotokana na katiba mpya inayotekelezwa nchini.
2. Subira huvuta heri.
3. Viwanda vina manufaa na madhara. Jadili.
4. "... Tangu siku hiyo nilifahamu fika kuwa, mtu yeyote anaweza kufanikiwa maishani bila kujali asili yake mradi tu awe na nidhamu na atie bidii katika chochote afanyacho."

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA GUCHA KUSINI
Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya (K.C.S.E)
102 / 2
KISWAHILI
KARATASI YA PILI

A. UFAHAMU (alama 15)

Soma makala yafuatayo Idsha ujihu maswali

Je wajua kwamba Kiswahili ni lugha ya sita ulimwcnguni na inatumiwa na watu zaidi ya milioni sita? Kiswahili hivi sasa kimewanda na kunawiri kila pembe ya dunia licha ya vizingiti vinavyoikumba katika uzambajazi wake.

Mbali na lugha za wageni, lugha ya Kiswahili ndiyo ya pekee ambayo chimbuko lake ni janibu ya pwani ya Afrika, Mashariki Kenya. Ni bayana kuwa lugha hii imevuka mipaka ya Afrika na inaenziwa na waja wa ughaibuni.

Lugha ya kigeni hasa Kiingereza ndiyo ilitumika kama lugha ya mawasiliano nchini Kenya kabla na baada ya uhuru. Walowezi walipuuza lugha ya Kiswahili na kuhimiza Kiingereza. Baada ya Uhuru, baadhi ya viongozi walioshika hatamu ya uongozi waliipigia debe Kiingereza na kuweka Kiswahili kapuni. Walidai eti Kiswahili ni lugha ya watu wasio na elimu na ustaarabu.

Mwasisi wa taifa la Kenya hayati Mzee Jomo Kenyatta anastahili mkono wa tahania kwa kuhimiza viongozi kuhutubia wananchi kwa lugha sanifu ya Kiswahili. Yeye mwenyewe hakuachwa nyuma, kwani hotuba zake nyingi ziliendelezwa kwa Kiswahili mufti, ili kukuza na kuendeleza Kiswahili miongoni mwa wakenya. Serikali iliteua tume ya kuchunguuza na kupendekeza mikakati ya kuimarisha elimu nchini. Tume hii iliongozwa na mpambe Msoni Ominde mwaka 1964. Baada ya utafiti, tume hii ilipendekeza kuwa lugha va Kiswahili iwe somo la lazima katika shule za msingi nchini. Viongozi mbalimbali tangu wakati huo wametoa maoni kababe kuhusu kukuza na kuendeleza Kiswahili, lakini vitendo vimekuwa haba mno. Watunga mitaala na sera za wizara va elimu tangu Uhuru, wamekuwa na mikatani ya kuyumbayumba kuhusu somo la Kiswahili katika viwango vyote vya elimu. Mathalani, somo la Kiswahili lilikuwa likilunzwa katika viwango vya shule za msingi hila kutahiniwa. Vipindi vya lugha hii vilikuwa, na hata sasa. Vichache mno vikilinganishwa na Kiingereza ambacho kimekuwa somo la lazima katika viwango vyote vya elimu na utahiniwa.

Chama cha KANU kilichokuwa uongozini wakati huo kilitoa mawazo mema kuhusu Kiswahili. Kwa mfano, 1969 azimio lilitolewa kuwa Kiswahili kiwe lugha ya taifa. kwa hivyo ilizizitizwa kitumiwe bungeni. Hali hii ndiyo ilipelekea sharti la wabunge kumaizi Kiswahili kabla kuteuliwa kuwania ubunge, llipendekezwa na katibu wa chama cha KANU kuwa ifikiapo mwaka 1974, Kiswahili kingekuwa lugha zote mbili zitumiwe kwa pamoja.

Rais mstaafu Daniel Arap Moi, alijaribu mno kukuza na kuendeleza lugha hii. Mikutano yake mingi iliendelezwa kwa Kiswahili. Kwa upande mwingine, nchini ya uongozi wake, sera mbalimbali kuhusu Kiswahili ziliibuka Kiswahili na kuiahiniwa katika viwango vya shule za msingi na za upili. Ni somo la lazima katika kiwango vya shule za msingi na za upili. Ni jambo la kutia moyo kwani Kiswahili kinafunzwa katika vyuo na shahada mbalimbali hutolewa.

Licha ya kuwa kuwa na vyombo vya habari vingi nchini, vipindi vingi hasa katika runinga na redio huendelezwa kwa Kiingereza. Magazeti ya Kiswahili ni haba mno. Hali hii hurudisha maenezi ya Kiswahili nyuma. "Mgalla mue na haki umpe" chambilecho wenye busara. Baadhi ya vyombo vya habari kama kipindi cha kamusi ya changamka" katika redio ya Nation ni kielezo bora cha kukuza lugha ni tukufu. Taarifa mbalimbali za habari katika vyombo hivi zimeimarisha mno lugha hii.

Mpaka leo, Kiswahili ni lugha ya wananchi wengi wa Kenya hata imevuka mipaka. Ni wazi kuwa ni lugha ya taifa na kimataifa na hivi karibuni kulingana na kielelezo bora cha katiba, itakuwa au imekuwa lugha rasmi, licha ya kutopewa hadhi inayostahili. Kiingcrcza bado ni lugha rasmi inayotumika katika shughuli mbalimbali. Tatizo kubwa linalokumba uenezaji wa Kiswahili nchini ni wingi wa viongozi ambao wamekua na kulelewa katika mazingira ya kigeni. Baadhi yao hufanya juu chini kutukuza Kiingereza. Huu ni ukengeushi usiofaa. Lugha ya mitaani kwa jina maarufu "sheng inafukuza badala ya kutukuza Kiswahili.

Iwapo lugha ya Kiswahili inaenziwa na wageni kama mashirika ya utangazaji kama BBC sauti ya Amerika na sauti ya China, seuze sisi Wakenya? Ni muhimu kuelewa kuwa mwacha mila ni mtumwa. Lugha hii ni yangu, yako na yetu. Ni chombo cha pekee cha kukuza na kuimarisha umoja wa kitaifa. Taifa lisilo na lugha ni sawa na mtoto asiye na mzazi. Tuvute

pamoja na tuhifadhi utamaduni wetu wa lugha.

a) Eleza njia nne zilizotumiwa na waasisi wa taifa la Kenya kukuza na kuendeleza Kiswahili. (alama 3)
b) Thibitisha ukitoa ushahidi kuwa Kiswahili ni lugha ya kimataifa. (alama 2)
c) Kuna vizingiti gani katika macnczi ya Kiswahili nchini Kenya? (alama 4)
d) Mwandishi wa makala haya anatoa mfano upi wa kutoa matumaini ya kuendeleza Kiswahili nchini Kenya. (alama2)
e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye habari. (alama 4)
Inaenziwa /Sera /Mikakati /Ughaibuni

2. UFUPISHO

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata

Katika safu yangu hii sina lengo la kuzishambulia dini zetu na namuomba Mungu sana asiniandikie dhambi kutokana na ninayotaka kuyaandika, lakini nashawishika kuikumbusha jamii yangu ambayo inatufanya watu tuziona dini zetu zinamkandamiza mwanamke.

Dini zetu kubwa kama Uislamu na Ukristo zinatuelekcza mwanamke kumheshimu mumewe na kumsikiliza anachosema. lakini kwa ycye kufuata maadili ya dini na si kukuambia uue ukakubali.

Wakati dini zinasema utekeleze amri ya mumeo na wao wameelekezwa mambo ya kuwafanyia wanawake, ikiwa ni pamoja na kuwaheshimu na kuwaridhisha kadri ya uwezo wao.

Kutokana na hilo la amri, wanaume wengi ndio wamechukua kama tiketi ya kumnyanyasa mwanamke na hata kumnyima fursa ya kujiendeleza kielimu au hata kufanya shughuli ya kuongeza kipato. Unakuta familia ni ya kimasikini, baba hana fedha za kutosha kuihudumia familia yake, lakini baba huyohuyo anataka mkewe asijishughulisha na shughuli yoyote ya kumuingizia kipato kinachoweza kuwasaidia wote na matokeo yake kuendelea kuwapo mwenye dimbwi la umasikini. Wcngine kwa hofu ya kupata changamoto kutoka kwa wake zao wanawakatalia wan awake waliowao kujiendelelza kiclimu au kutafuta mwanamke asiyeelimika ili asiweze kuhoji mambo kadha ndani ya nyumba.

Hili limebainishwa hivi karibuni na shirika moja lisilo la kiserikali huko Kigoma ambapo katika utafiti wao wanasema asilimia 90 ya wan awake wa vijijini wanashindiwa kutoa hoja kutokana na uelewa wao kuwa duni kutoa sababu ya kuwa hivyo ni kutokana na ukosefu wa elimu, masuala ya kidini yanayomuelekeza mwanamke kufuata amri za mumewe, mila na desturi kadhaa.

Dini zote zinaeleza wazi umuhimu wa mtu kupata elimu bila kubagua kama ya kiislamu inavyosema mtu anapata thawabu anapotafuta elimu na anatakiwa aitafute popote bila kujali umbali na hata ikiwezekana kufika china ambapo inaaminika ni mbali.

Sijawahi kuona wala kusikia dini ikisema mwanamke asipate elimu lakini baba zangu na kaka zangu, wanaume wanaliptosha hili na kutaka kuendelea kumkandamiza mwanamke bila kufikira kuwa mwanamke ni msaada mkubwa kwao na kwa maendeleo ya taifa lolote. Ikiwa leo tupe katika harakati za kupata maendeleo na nchi hii, hi vi kweli tutafanikiwa?

Mapambano ya kuleta maendeleo yaanze katika ngazi ya familia kwa kuondokana na ujinga wa kumkadamiza mwanamke iii naye aelemike, aweze kujenga hoja, aweze kujitafutia kipato na mwisho kusadidia katika maendeleo ya familia ambayo kwa njia nyingine ndiyo maendeleo yeneywe ya taifa hii.

a) Huku ukirejelea aya nne za kwanza za makala haya, onyesha nanma dini inatumiwa kukandamiza watu. (Mtiririko 2) (alama 6 - maneno 50 - 70)
Matayarisho/Jibu
b) Mwanamke anaweza kuendelezwa kivipi ukirejelea aya mbili za mwisho za makala haya. (maneno 40)
Matayarisho/ Jibu (alama 6)

3. **MATUMIZI YA LUGHA.** (alama40)

a) Yakinisha
Usipofanya bidii hutafaulu (alama 2)
b) Andika kwa wingi (alama 1)
Uzee umemsumbua sana
c) Tofautisha kati ya suati ghuna na sighuna. (alama2)
d) Changanua sentensi ifuatayo kwa mishale.
Wanafunzi waliogoma juzi wamefukuzwa. (alama 4)
e) Tunga sentensi tatu ili kuonyesha maana tofauti ya neno 'vua' (alama 3)
f) Tumia viambishi vikanushi -ja- nu - i - katika sentensi. (alama 2)
g) Tunga sentensi ukitumia kiunganisha ‘maadamu’ (alama .2)
h) Unda vitenzi kutokana na nomino zifuatazo.
i) Mtukufu (alama 1)
ii) Mchumba (alama 1)

i) Tambua aina za viclezi vilivyopigiwa mstari.
   a) Mtoto alikimbia upesi (alama l)
   b) Juma alipigwa sana (alama 1)
j) Eleza matumizi mawili ya mtajo . (alama 2)
k) Andika katika mscmo wa taarila.
   Nitakuwa nikija hapa shulcni kukuona .' Mzazi alimwambia mtoto wake. (alama 3)
l) Eleza matumzi ya kwa katika sentensi ifuatayo.
   Wageni walifika kwangu jana kwa gari lao. (alama 2)
m) Andika udogo wa sentensi ifuatayo.
   Kiti chake kimevunjika . (alama 1)
n) Tunga sentensi ukitumia kitenzi 'paka' katika jinsi ya kutendata . (alama 2)
o) Onyesha matumizi tofauti ya ingine katika sentensi. (alama 2)
p) Andika sentensi ifuatuyo katika wakati unaotarajiwa.
   Watoto walikula mihogo (alama 2)
q) Eleza tofauti katika sentensi zifuatazo
   Ningalishinda ningalisherehekea
   Ningeshinda ningesherehekea. (alama 2)
r) Tambua aina ya kihusishi kilichopigiwa mstari.
   Tutafagia kutoka ukumbi hu hadi ule. (alama 1)

4. ISIMU JAMII

Eleza tofauti kati ya lugha ya maandishi na lugha ya mazungumzo. (alama 10)

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA GUCHA KUSINI
102 / 3
KISWAHILI
Karatasi ya Tatu

SEHEMUYA A: TAMTHILIA
MSTAHIKI MEYA . T. M. Arege

1. Si nyinyi ndio mjuao wanangu! Mimi sifahamu ila nilikiona afadhali.
a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Taja tamathali iliyotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)
c) Eleza kwa undani maisha ya msemaji. (alama 8)
d) Taja na ueleze maudhui mawili yanayoendelezwa na dondoo hili. (alama 6)

SEHEMUYA B: RIWAYA
UTENGANO S.A. Mohammed
Jibu swali la 2 au la 3

2. Lakini hatimaye alinyamaza na kilio chake kilikatika moja kwa moja, na chozi lake, lile alililoliita. 'Chozi la mliwa' lilikauka moja kwa moja pia.'
a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b) 'Chozi la mliwa' (alama 2)
i) Mliwa ni nani; analiwa na nani?
ii) Elezajinsi alivyoliwa. (alama 14)
3. Huku ukitoa mifano mwafaka, Jadili jukumu la mwanamke katika riwaya ya *Utengano* (alama 20)

SEHEMU YA C HADITHI FUPI
Jibu swali la 4 au la 5
Damu Nyeusi na Hadithi nyingine! Ken Walibora na S.A. Mohamed.

4. Hadithi: *Samaki wa nchi za joto.*
a) Onyesha aina mbalimbali za dhuluma katika hadithi hii. (alama 5)
b) Onyesha athari za kimagharibi katika hadithi hii. (alama 5)
c) Mwandishi ana maoni gani kuhusu elimu. (alama 5)
d) Taja maovu mbalimbali yanayoangaziwa katika makala haya. (alama 5)

AU

5. Jadili aina mbalimbali za ubaguzi unaoendelezwa Marekani kama inavyosawiriwa katika Hadithi ya *Damu Nyeusi.* (alama 20)

SEHEMUYA D

6. **USHAIRI.**
Shairi A
1. Jaribu kuwa mpole, kwa wenzio darasani,

jihadhari na kelele, na utusi mdomoni,
wala siwe kama wale, wanafunzi maluuni,
Waso akili viehwani, katu usiwaingilie.

2. Ujipanyapo ja vile, watoto wale wahuni,
Juwa jatakwenda mbele, utashindwa mtihani,
Na toka dakika ile, utaingia mashakani,
Jaribu uwe twaani, mwanafunzi zingatile

3. Mtoto kiwa mpole, nakueleza yakini,
Huwa ni mfahamile, wa elimu akilini,
Ni shida kuangukile, kushindwa na mtihani,
Yataka utamakani, mwanafunzi siliwale.

4. Mwanafunzi nakukanya, kwa yale mawi mwandani
Sizowee kusengenya, sengenyo mashakani,
Kama hilo ukifanya, utakuwa madhakani,
Ni hayo nilowaonya, kwa hivyo nawaageni.

Shairi B

Aliniusia babu, zamani za utotoni
Kanambia jitanibu, na mambo ya nuksani
Na wala usijaribu, kwa mbali wala jirani
Malifi ni duniani, kuzimu kwenda hisabu.

Liche jambo la aibu, lipalo mtu huzuni
Liuvunjao wajibu, m'bora akawa duni
Lau chamba utatubu, kulipwa hukosekani
Malifi ni duniani, kuzimu kwenda hisabu

Usipolipwa karibu, lakutoka fahamuni
Lazima lije jawabu, ingawa pindi mwakani
Japo kuwa ughaibu, au mwisho uzeeni
Malifi ni duniani, kuzimu kwenda hisabu.

Kila neno lina jibu, usitafute kwa nini
Mambo yenda taratibu, pupa jingi lafaani
Akopeshae zabibu, atalipwa zaituni
Malifi ni duniani, kuzimu kwenda hisabu

Ahimilie taabu, hupata merna mwishoni
La raha au sulubu, malifi ni duniani
Mambo bahati nasibu, viumbe tahadharini
Malifi ni duniani, kuzimu kwenda hisabu.

Maswali:

a) i) Linganisha shairi Ana B kwa kuzingatia maudhui (alama 6)
ii) Linganisha na kutofautisha mashairi A na B ukizingatia sifa za arudhi. (alama 6)
b) Toa mifano miwili yoyote ya inkisari kutoka kwa mashairi haya. (alama 2)
c) Fafanua maana ya mishoro ifuatayo kama ilivyotumiwa katika mashairi haya. (alama 2)
i) Kanambia jitanibu. na mambo ya nuksani.
ii) Mwanafunzi nakukanya, kwa yale mawi mwandani.
d) Eleza maana ya msamiati ufuatao (alama 4)
i) Nuksani ii) Sulubu iii) Malifi iv) Katu

FASIHI SIMULIZI.

7. a) Taja sifa zozote NNE za maigizo. (alama 4)
b) Taja aina zozote NNE za maigizo. (alama 4)
c) Ni nini tofauti ya maagizo na hadithi? (alama 6)
d) Taja sifa SITA za mwigizaji bora. (alama *6)*

MTIHANI WA PAMOJA WA ENEO GATUZI LA KAJIADO , 2013
Cheti Cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/1
KISWAHILI

KARATASI 1
Muda: Saa 1¾

1. Wewe ni katibu wa kamati ya usalama katika eneo gatuzi lenu. Usalama umedorora katika eneo hili. Andika ripoti inayopigia darubini swala hili.
2. Migogoro ya kifamilia huchochewa kutoka nje. Jadili
3. Andika insha kuhusu methali.
Usipoziba ufa utajenga ukuta.
4. Andika kisa kitakachoishia kwa maneno haya .
..... Ama kwa kweli hapo ndipo nilipogundua kuwa nadharia isemayo kwambajirani ni nduguyo ni potovu

MTIHANI WA PAMOJA WA ENEO GATUZI LA KAJIADO , 2013
Cheti Cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/2
KISWAHILI
KARATASI 2
Muda: Saa 2½

1. UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

MAGEUZI yanayotarajiwa katika idara ya polisi nchini yameanza kubisha hodi baada ya kuzindliwa kwa mtaala mpya wa kutoa mafunzo kwa maafisa wa polisi.

Mtaala huo uliozinduliwa rasmi na Waziri wa Usalama wa ndani Prof. George Saitoti Jumatatu iliyopita unalenga kuimarisha utendekazi katika kikosi ambacho kwa muda mrefu kimelaumiwa kwa kukolewa ufisadi na uvunjaji wa haki za kimsingi.

Akihutubu katika hafia ya kuzindua mtaala huo, iliyofanyika akatika makao makuu ya shirika la ndege nchini mtaani Embakasi, Nairobi, Jumatatu iliyopita. Waziri Saitoti alisema kuzinduliwa kwa mtaala huo kuliashiria mwanzo wa mageuzi makubwa yanayonuiwa kukipatia kikosi hicho sura mpya.

"Nyakati zimebadilika na tutawapatia maafisa wa polisi mafunzo mapya. Tunataka kuunda kikosi imara, chenye nidhamu, kinachoheshimu haki za kibinadamu.

Tunataka kuwa na kikosi kinachoakisi sura ya kame hii na kinachoafikia hadhi ya kimataifa.' Waziri Saitoti alisema.

Mtaala huo mpya wa kutoa mafunzo kwa maafisa wa polisi ni matunda ya jopo iliyoteuliwa na Rais 2003, kutathmini mageuzi aktika kikosi hicho. Uliandaliwa na taasisi ya elimu nchini ikishirikiana na wakufunzi kutoka chuo cha mafunzo ya polisi ya Kiganjo kwa usaidizi wa wataalamu wa maswala ya usalama kutoka Uswizi.

Chini ya mtaala huo, maafisa wa polisi watapokea mafunzo kwa kipindi cha kati ya miezi 15 na 21 kinyume na awali ilipowachukua miezi 9 tukukamilisha mafunzo,

Aidha, alama za kujiunga na kikosi hicho zimeongezwa. Katika mtaala huo, wanaonuia kujiunga na idara ya polisi wa kawaida, kitengo cha GSU au polisi wa utawala, ni lazima wawe wamepata alama ya C katika mtihani wa KCSE na itawachukua miezi 15 kukamilisha mafunzo ikiwa ni pamoja na miezi 3 ya kujifahamisha na huduma za kikosi.

Hii ni tofauti na awali ambapo alama ya kujiunga na kikosi cha polisi ilikuwa ni D katika KCSE. Mtaala mpya unasema ni sharti asilimia 10 ya makurutu wawe digrii kutoka chuo kikuu na watapokea mafunzo kwa miezi 21 na kuhitimu cheo cha naibu inspekta wa polisi.

Na kuanzia sasa ni sharti usawa wa kijinsia uzingatiwe kikamilifu katika uajiti wa maafisa wa polisi.
Wachangamuzi wa masuala ya usalama wanasema ukizingatiwa ipasavyo, mtaala huo utasaidia kuunda msingi dhabiti wa kikosi imara ambacho wakenya wamekuwa wakihitaji.

Maswali

a) Ni dalili ipi inayoonyesha mwanzo wa mageuzi? (alama 1)
b) Mtaala mpya unalenga nini? (alama 4)
c) Eleza lawama zinazoelekezewa kikosi cha polisi. (alama 2)
d) Kwa mujibu wa kujifunga eleza mambo matatu yanayokusudiwa kuletwa na mtaala mpya. (alama 2)
e) Taja makundi mawili yaliyohusika katika kuandaa mtaala mpya. (alama 2)
f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu. (alama 3)
   i) Kubisha hodi
   ii) Kukolewa
   iii) kinachoakisi

2. UFUPISHO

Soma taarifa hii kisha ujibu maswali

Katika siku za hivi majuzi, vijana wawili wa kiume wanaofahamika humu nchini wamegonga vichwa vya bahari kwa kujitokeza hadharani wakifunga ndoa. Mijadala mikali ikazika huku vidole vya lawama vikinyooshwa pande zote: si kwa walimu, si kwa viongozi wa kanisa. Swali kubwa likawa kwa nini? Jamii nzima ilijitosa kwenye soga la kutafuta kilichosababisha upotovu wa maadili wa kiwango kikubwa kama hicho.

Hisia za kimapenzi baina ya watu wa jinsia moja zaweza kuchipuka kutokana na sababu mbalimbali. Wazazi wana mchango mkubwa katika kuwalea watoto na kuwazingatisha maadili faafu. Mtoto umleavyo, ndivyo akuavyo. Ni muhimu mzazi amfunze mtoto kuhusu desturi za jamii na matarajio yake. Katika jamii za kisasa.viwango vya 'maendeleo ' na 'ustaarabu' hupimwa kwa kutumia mizani ya kuiga desturi za kigeni. Tume bobea mno kwenye sarakasi ya kuiga uzungu hadi tukajisahau na kuuzika utamanduni wetu! Yeyote anayewania kuuendeleza huitwa mshamba, asiyefaa kuyaona mapambazuko.

Baadhi ya vijana hudai kushawishiwa na donge nono wanazodhani zitawakwamua kutoka giza la ukata. Yadaiwa kuwa ngono ya jinsia moja ina mali chekwachekwa. Kutokana na tatizo la uhaba wa kazi, ambalo limesambaa ulimwenguni kote si ajabu vijana wakavutiwa kwenye mkondo huo wa maisha. Vile vile, kunao vijana wa kiume wanaodai kuwa, gharama ya kukidhi matarajio ya wasichana wa rika lao ni ya juu mno, ilhali wavulana hao hawana ajira. Basi, badala ya kusononeka kwa kukataliwa na wasichana, heri wapendane na wanaume wenzao! Lakini je, haya yote huanzia wapi? Wateja wengi katika biashara hii hukiri kuianzia shuleni, hasa shule za mabweni. Inadaiwa kuwa uhusiano wa aina hii umeenea kwa viwango vya kutisha shuleni. Walimu huwa wapi wakuwakanya?

Vijana wengi huhusiana kimapenzi kisiri, kiasi cha kula yamin wasitambuane. Sababu hasa ni kuwa, mapenzi ya aina hiyo hayana hofu ya mmoja wao kupata mimba. Isitoshe, ni njia rahisi ya kujifurahisha na kuliwazana hasa wanapolemewa na mzigo mzito wa usomi. Ikichukuliwa kuwa wazazi wengi hawana muda wa kuwashauri vijana, ni rahisi zaidi kuingilia uozo huu. Ajabu ni kuwa, baadhi ya vijana wanadai kuingilia ufasiki huu kwa kushawishiwa na wazazi wao au walezi!

Mapenzi ya jinsia moja yanaweza kulemaza hisia za kimapenzi baina ya mke na mume.Kijana aliyeingilia mkondo huo hushindwa kuhusiana kwa njia ya kawaida kimaumbile na mwenzake wa ndoa katika siku za baadaye. Anaweza pia kuchekelewa na kudhihakiwa kiasi cha kutoweza kujiamini lena. Aila yake yaweza kuaibishwa na hata kutengwa na jamii nyingine. Ugonjwa wa ukimwi huweza kusambazwa kwa kasi has a iwapo wahusika hawatumii mipira ya ngono. Hivyo basi, kuiga kila jambo geni si fahari. Tufahamu kuwa ni vizuri kuthamini mila na desturi zetu kwani, mwacha mila ni mtumwa.

Maswali

1. Eleza sababu zinazochangia kuchipuka kwa hisia za kimapenzi baina ya vijana wa jinsia moja. (maneno 60-65) (alama 9)
   Nakala chafu
2. Kuna hatari gani za kushiriki ngono baina ya vijana wajinsia moja. (maneno 25-30) (alama 6)
   Nakala chafu/Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) Vitamkwa vifuatavyo ni vya aina gani? (alama 2)
i) /ng'/
ii) /r/
b) Onyesha mofimu katika maneno haya. (alama 2)
i) Darasa
ii) Mtoto
d) Tunga sentensi kwa kutumia neno 'mpaka' kama: (alama 2)
e) i) Nomino
ii) Kihusishi
d) Nomino 'ua' hujitokeza katika ngeli mbili tofauti. Zitaje. (alama 2)
e) Andika kwa wingi (alama1)
Karatasi ii hii ni ghali
f) Bainisha matumizi ya "ni' katika sentensi zifuatazo. (alama 3)
i) Simameni
ii) Kamau ni kijana hodari
iii) Wamenikaribisha.
k) Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo
Mwanafunzi anazungumza kiingercza vizuri sana. (Tumia **wakati usiodhihirika)**
h) Nyambua vitenzi vifuatavyo kulingana na maagizo. (alama 3)
i) lewa **(tendea)**
ii) nywa **(tendeana)**
iii) waka **(tendesha)**

i) Andika nomino kutokana na vitenzi hivi. (alama 1)
   i) Nasihi
   ii) Arifu
j) i) Kishazi ni nini? (alama 1)
   Tumia neno 'imba' katika sentensi kuonyesha
   ii) Kishazi huru
   iii) Kishazi tegemezi
k) Tofautisha maana kutika sentensi hizi (alama 2)
   i) Nina wajibu
   ii) Ninawajibu.
l) Andika kwa usemi halisi. (alama 3)
   Tajiri alishangaa jinsi alivyoweza mzigo huo peke yake.
m) Changanua sentensi hii kwa kutumia matawi. (alama 4)
   Baba, mama na ndugu yake watatenda Kitale kesho.
n) Tunga sentensi mbili kuonyesha maana tofauti za neno oza. (alama 2)
o) Andika kinyume cha: (alama 2)
   Baba Fatuma aliingia nyumabani polepole.
p) Kanusha sentensi ifuatayo. (alama 2)
   Kucheza kwake kumewafurahisha wengi.
q) Andika sentensi ifuatayo kwa udogo wingi. (alama 2)
   Mtoto yule anajaribu kuchora kitabu kwa kijiti.
r) Eleza matumizi mawili ya alama ya mshazari. (alama 2)

4. ISIMUJAMII

Ngoma hii inawabamba sana wasee. Imeshika mpaka hata watoi mtaani wanaielewa.
Nangos mob zinaitumia kama 'skiza tune'. Sikiza kwa sekunde 5.

a) Taja sajili inayorejelewa hapa. (alama 1)
b) Huku ukirejelea kufungu hiki eleza sifa nne za sajili uliyotaja. (alama 4)
c) Eleza dhana ya ujozilugha huku ukitoa mfano mmoja. (alama 2)
d) Eleza istilahi zifuatazo kama zinazotumiwa katika isimu jamii. (alama 3)
i) Misimu
ii) Lafudhi
iii) Pijini

MTIHANI WA PAMOJA WA ENEO GATUZI LA KAJIADO , 2013

Cheti Cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)

102/3

KISWAHILI

KARATASI 3

Muda: Saa 2½

SEHEMU YA A:

SWALI LA LAZIMA .(UTENGANO - S.A MOHAMMED)

1. " …Bado Afrika inatawaliwa ..... Utawala mamboleo wa nje kule utokeapo
   Na ndani uendelezwako ..... "
a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b) Taja na eleze sifa mbili za aliyetoa kauli hii. (alama 4)
c) Thibitisha kuwa bado "ukoloni" mamboleo unaendelezwa nje na ndani katika jumuiya ya utengano. (alama 12)

TAMTHILIA:

Mstahiki Meya (Timothy Arege)

2. "Juzi mtoto wa Kerekecha amekufa kama nui. Amemfia mikononi mwake mwenyewe Kerekecha akitazama. Sisi tunaambiwa hakuna dawa na zinapokuwa ….."
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Taja na ueleze sifa tatu za masemaji wa maneno haya. (alama 6)
c) Kwa kutolea mfano, taja tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
d) Jadili mikakati yoyote minne iliyotumika kukomboa mji wa Cheo. (alama 8)
3. Mwandishi wa tamthilia ya Mstahiki Meya amefaulu katika kutumia mbinu za majazi na ishara.
   Huku akitoa mifano mitano thibitisha ukweli huu. (alama 20)
4. **USHAIRI**

Fanya swali la 4 au la 5

Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

1. Dunia kitu dhaifu, si ya mtu kunyetea,
   Usione ufanifu, na furaha kila njaa,
   Kumbuka na uvunjifu, kama ndwele hukujia,
   Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

2. Anasa usiandame, kwa pupa kuzipapia,
   Heri moyo fanye tume, uche kuzikimbia,
   Hakuna mume wa dume, na wala hatatokea,
   Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

3. Wako wapi mashujaa, wenye nguvu kila njia,
   Ziliwafika nazaa, wakabaki kujutia,
   Ndunia ina hadaa, yataka kuzingatia.
   Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

4. Kam kam mahuluki, viumbe vyake jalia,
   Walokuwa na maluki, bora za kujivunia,
   Muda wakitahamaki, iliwatupa dunia,
   Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

5. Fikiri zao sharafu, walizo wakitumia,
   Penye unasi alifu, wanenalo maridhia,
   Mwisho wayo madhaifu, na majina kupotea,
   Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

6. Walishushwa ghorofani, mapambo na mazulia,
   Wakawachia wandani, na mali zilizosalia,
   Wameshia kaburini, udongo kuwafukia,
   Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

7. Natarudi kwa manani, tutubu zetu hatia,
   Kwa baraka za Amini, Mola tatughofiria,
   Tutafuzu duniani, mema na ahera pia,
   Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

8. Turudipo kwa Jalali, tukayawacha mabaya,
   Kila sada tutanali, na shairi kutwepushiya,
   Tutapata na uvuli, ahera kujifichiya,
   Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

Maswali

a) Pendekeza anwani mwafaka kwa shairi hili (alama 1)
b) Taja na ufafanue mifano yoyote minne ambayo mshairi ametumia kusisitiza ujumbe wake. (alama 4)
c) Huku ukitoa mifano eleza idhini ya mtunzi kama inavyojitokeza katika ubeti wa nane. (alama 8)
d) Taja na ueleze mbinu mbili za kifasihi zilizotumika mkatika shairi hili. (alama 2)
e) Eleza muundo wa ubeti wa tatu wa shairi hili ukizingatia mizani na vina. (alama 2)
f) Andika ubeti wa sita katika lugha nathari. (alama 4)
g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 3)

i) Kam kam
ii) Tutaghofiria
iii) Madhaifu

5. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yote.

Kazi ni kazi
Kazi inozaa mazao
Kazi mbii hakuna
Kazi ni uhai
Kazi hukuza uchumi.

Kazi haiwi kazi
Kazi paso uhai
Kazi msingi wa maisha
Kazi huleta maendeleo.

Kazi ni baraka
Uhai ni baraka
Uhai ni kazi.

Kazi usofanya
Baraka takosa
Na uhai vilevile.

Kokoiko! Kucha kuchele Kengele ngelengele
Kiumbe wamaka
Kumekucha! Kazi kihofia
Kusudi blangeti tavuta
Kujigubika gubugubi
Kujisingizia ndwele.

Kazi mzembe hutamani
Ni damuyo kuilaza
Na kuupiga uvivu

Kazi kutotamani fahamu
Ni kutamani mauti
Na mauti yakikufika
Ole mbwako tajijutia!

MASWALI

a) Tambua hili ni shairi la aina gani na uthibitishe. (alama 2)
b) Utungo huu unadhihirisha sifa zipi za kishairi? (alama 4)
c) Taja sifa nne za mtu mzembe kwa mujibu wa shairi hili (alama 4)
d) Eleza ujumbe wa shairi hili. (alama 3)
e) Taja na utoe mifano ya tamathali zozote mbili za lugha zilizotumiwa katika ubeti wa kwanza. (alama 4)
f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika ushairi. (alama 3)
i) Kazi mbii
ii) Wamaka
iii) Ndwele

HADITHI FUPI
(DAMU NYEUSI na Hadithi nyingine) KEN WALIBORA

6. Eleza nafasi ya mwanamke katika hadithi zifuatazo: (alama 20)
i) Mke wangu
ii) Samaki wa nchi za joto
iii) Damu Nyeusi
iv) Glasi la mwisho makaburini.

FASIHI SIMULIZI

7. a) Eleza sifa za ngano (alama 4)
b) Eleza sifa tano za migani (alama 4)
c) Eleza maana ya vipera hivi. (alama 8)
i) Visaviini
ii) Tarihi
iii) Kumbukumbu
iv) Hurafa
d) Eleza dhima ya ngano za mazimwi
(alama 4)